Mashamba Makubwa ya Miti kwa ajili ya Viwanda

YANAVYOVAMIA

Mashariki na Kusini mwa Afrika

World Rainforest Movement

TIMBERWATCH COALITION

Shukrani

Taarifa hii iliandaliwa na shirika la Vuguvugu la Misitu ya Mvua Duniani yaani The World Rainforest Movement (WRM) na Umoja wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na watu binafsi wanaoangalia Maswala ya Mbao wa The Timberwatch Coalition (TW), kwa msaada mkubwa kutoka kwa watu wa kujitolea ambao walishauri au kusaidia kwa njia mbalimbali.

Picha na Timberwatch na WRM

Michoro ya Jalada na Awesome

Kazi hii iliwezekana kupitia michango kutoka Mfuko wa Ruzuku ya Kijani wa Dunia wa the Global Greengrants (GGF), Misereor (Ujerumani), na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa (Sida) kupitia Shirika la Utunzaji wa Mazingira la Jamii ya Waswidi la the Swedish Society for Nature Conservation (SSNC).

Maoni yaliyotolewa katika nyaraka hii si lazima yatafakari mitizamo na maoni ya wachangiaji au wafadhili wao.

WRM – International Secretariat
Avda. Gral María Paz 1615/3 CP 11400, Montevideo
Uruguay. Ph: +59826056943
E-mail: wrm@wrm.org.uy
Website: http://wrm.org.uy

Timberwatch Coalition (South Africa)
Project co-ordination office
91 Springside Rd, Hillcrest Park 3610,
South Africa. Ph. +27824442083
E-mail: timberwatch@iafrica.com
Website: www.timberwatch.org

Mashamba makubwa ya zao moja la miti husababisha madhara mengi hasi ya kijamii na kimazingira. Mwaka 2004, katika mkutano wa mtandao wa jamii wa harakati dhidi ya mashamba makubwa ya miti katika Brazil, Septemba 21, 'Siku ya Kimataifa dhidi Mashamba Makubwa ya zao moja la miti' ilizinduliwa kama kampeni ya kila mwaka ya asasi za kiraia kutaka kutokomezwa kwa upanuzi wa kimataifa wa mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda.

Tafadhali shiriki! Angalia hapa kwa maelezo zaidi:
http://wrm.org.uy/highlighted_post/international-day-of-struggle-against-monoculture-tree-plantations-2017

Septemba 2017

Mashamba makubwa ya miti
Kwa ajili ya viwanda yanavyovamia
Mashariki na Kusini mwa Afrika

YALIYOMO

1. **Utangulizi**
2. **Taarifa za nyuma/usuli**
3. **Mashamba makubwa ya miti yaliyopo sasa na baadaye**
4. **Wanaoendesha upanuzi wa mashamba makubwa ya miti**
5. **Harakati za jamii dhidi ya mashamba makubwa ya miti**
6. **Hitimisho**

Kiambatanisho: Taarifa za nchi kwa kanda

a) Afrika Kusini, Swaziland na Lesotho (Kusini)
b) Malawi, Msumbiji, Zambia na Zimbabwe (Kati)
c) Kenya, Tanzania na Uganda (Kaskazini)
d) Madagascar (Mashariki)

TIMBERWATCH COALITION

World Rainforest Movement

1. Utangulizi

Taarifa hii ya pamoja kati ya Timberwatch Coalition (TW)[1] na World Rainforest Movement (WRM)[2] inalenga katika mambo mbalimbali ya ndani na nje yanayojulisha kuhusu hali ya mabadiliko ya mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda katika nchi 11 za Mashariki na Kusini mwa Afrika. Kwa mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda (ITPs), tuna maana mashamba makubwa ya miti ya aina moja yanayosimamiwa kwa umakini, yenye umri unaolingana mingi ya hiyo ni ya jamii ya mikaratusi, misindano au migunga (acacia) ambayo siyo ya asili, ambayo imepandwa kwa lengo kuu la kupata timbao kwa ajili ya mchakato wa uzalishaji viwandani, au kwa ajili ya shughuli nyingine za biashara kama vile biashara katika kaboni inayoongezeka.

Kama sehemu ya tatizo pana la uporaji wa ardhi, mataifa ya Kusini yanaonekana na wageni, ambao wengi wao ni wawekezaji wa Kaskazini, kama mahali panapovutia na kutengeneza faida kiurahisi kwa kubadilisha inayodhaniwa kuwa 'ardhi isiyotumika' kuwa mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda. Maeneo ya Afrika ambayo yako kwenye uchambuzi, hasa nchi za pwani kama Msumbiji, yanavutia walanguzi wa kigeni kwasababu yana hali ya hewa ya kufaa zaidi na aina ya ardhi kwa ajili ya mashamba makubwa ya miti, zaidi ya kuwa yamekaa vizuri kulifikia kiurahisi soko la mbao la Asia. Utafiti huu unachunguza upanuzi wa mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda na waendeshaji wake wa nje, pamoja na changamoto zilizotolewa na upanuzi huu kwa jamii za ndani zilizoathiriwa zinavyojitahidi kulinda ardhi na maisha yao.

Lengo la zoezi hili kijiografia ni pamoja na maeneo yaliyomo Mashariki na Kusini mwa Afrika ambapo Uingereza, koloni kubwa la wakati huo, lilikuwa tayari limeanzisha baadhi ya mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda mwishoni mwa karne ya 19. Hii ni pamoja na Afrika Kusini, ambayo kwa sasa ina eneo kubwa zaidi chini ya mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda katika bara zima. Nchi jirani ya Msumbiji, zamani koloni la Ureno, ina uzoefu wa kiwango cha kasi zaidi cha upanuzi mashamba makubwa ya miti zaidi ya miaka 5-10 iliyopita. Nchi nyingine tisa zilizomo ndani ya wigo wa utafiti huu ni pamoja: Kenya, Tanzania, Uganda, Malawi, Zimbabwe, Zambia, Swaziland, Lesotho, na Madagascar, ambayo ilikuwa koloni la Ufaransa.

Kwa mujibu wa takwimu rasmi za (FAO), ilipofika mwaka 1990 nchi hizi 11 tayari zilikuwa zina jumla ya hekta milioni 2.7 zilizo chini ya mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda. Wakati huo huo, kulikuwa na takribani hekta milioni 7 katika Afrika nzima, zinazowakilisha chini kidogo ya 10% ya jumla ya eneo la mashamba makubwa ya miti Kusini mwa dunia[3]. Katika miongo michache iliyopita, mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda yameongezeka zaidi kwa kasi katika Kusini mwa dunia kuliko katika Kaskazini mwa dunia. Hii ni kutokana na sababu kadhaa ambazo zimefanya hivyo kuwa kuvutio zaidi kwa makampuni na wawekezaji kuanzisha mashamba mapya ya miti Kusini mwa dunia, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa ardhi na nguvu kazi kwa gharama nafuu, sheria zisizokuwa kali za mazingira, na viwango vikubwa zaidi vya ukuaji wa miti kuliko kwa mfano katika Amerika ya Kaskazini na Ulaya[44]. Kutoka mwaka 1995, eneo lililo chini ya mashamba ya miti kwa ajili ya viwanda katika nchi 11 zilizojumuishwa katika tathmini hii liliongezeka kutoka lililotajwa hapo mwanzo la hekta 2.7 milioni mwaka 1990, mpaka hekta milioni 3.4 mwaka 2015, ongezeko la 25%. (Angalia Jedwali katika ukurasa wa 9)

Taarifa hii ina lengo la kusaidia kueleza kwanini hali hii ya upanuzi ipo, kwa kutambua waendeshaji wake na matokeo yake, na kusambaza taarifa hii na taarifa nyingine muhimu miongoni mwa mashirika ya ndani, kitaifa, kikanda na kimataifa na watunga sera ndani na nje ya Afrika. Lengo ni kujenga uelewa mkubwa wa umma wa kiasi cha ongezeko la athari mbaya zinazosababishwa na miradi yote iliyopo na mipya inayoweza kuazishwa ya mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda katika nchi zilizoathirika, na kutahadharisha wadau wote kuhusu mwenendo huu, ikiwa ni pamoja na vitisho na changamoto inazosababisha kwa jamii ambazo ardhi yao inalengwa na wawekezaji wa kigeni wa mashamba makubwa ya miti na makampuni ya usindikaji wa timbao.

---

[1] www.timberwatch.org
[2] www.wrm.org.uy
[3] FAO Forest Plantations Working Papers - *TROPICAL FOREST PLANTATION AREAS - 1995 DATA SET* - Based on the work in 1997 of D Pandey, Consultant, Edited by M. Varmola and A. Del Lungo, May 2002 ftp://ftp.fao.org/docrep/fao/006/Y7204E/Y7204E00.pdf
[4] Overbeek W, Kröger M, Gerber J.F. 2012. An overview of industrial tree plantation conflicts in the global South. Conflicts, trends, and resistance struggles. EJOLT Report No. 3, p.100

Aelezo ya jumla ya taarifa hii

Kufuatia utangulizi na maelezo (sura ya 1), sura ya 2 inatoa historia fupi ya jinsi mashamba makubwa ya miti yalivyokuja mashariki na kusini mwa Afrika. Sura ya 3, inajumuisha jedwali linaloonyesha takwimu za serikali za maeneo ya mashamba makubwa ya miti katika nchi 11 zilizojumuishwa chini ya wigo wa taarifa hii, pamoja na makadirio ya uwezekano wa upanuzi wa baadaye katika kipindi hadi kufikia mwaka 2035.

Katika Sura ya 4, michakato ya kisiasa na mambo mengine yanayoendesha upanuzi wa mashamba makubwa ya miti katika nchi husika, pamoja na malengo ambayo mashamba mapya ya miti yanaanzishwa, yanaelezewa na kutolewa maoni.

Sura ya 5 inagusia baadhi ya changamoto kuu ambazo jamii inakutana nazo pindi wanapokumbana na makampuni ya mashamba makubwa ya miti 'yanayonyang'anya', na mifano ya jamii ambazo tayari zina uzoefu wa uvamizi wa ardhi na maisha yao unaofanywa na mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda. Hii inafuatiliwa na maoni ya kuhitimisha katika sura ya 6.

Katika sehemu ya kiambatanisho, chambuzi fupi za hali inayohusiana na mashamba makubwa ya miti katika kila moja ya nchi 11 zinajumuishwa, kwa kutaja baadhi ya miradi mikuu ya mashamba makubwa ya miti inayoendelezwa, watendaji wanaohusika, na taarifa nyingine muhimu.

Kutoa taarifa ambayo wakati huo huo inapitia habari zitumiwazo katika kufikia hitimisho kutoka nchi kadhaa tofauti si kazi rahisi, kwasababu mara nyingi ni vigumu kupata habari za kuaminika. Taarifa hii inapaswa kutazamwa zaidi kama 'mradi unaoendelea', kuliko ripoti iliyohitimishwa. Maoni yoyote ya msomaji, au taarifa yoyote mpya au ya nyongeza inayohusiana na nchi 11 zilizo kwenye uchambuzi, vile vile kutoka nchi nyingine za Afrika ambazo hazijajumuishwa, yatakaribishwa. Msaada huu utafanya iwezekane kushirikishana habari zaidi zinazohusiana, na kujulikana zaidi kwa suala linaloendelea la upanuzi wa mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda barani Afrika. Pia itatusaidia kuchapisha habari mpya, kwa lengo la kusaidia wanajamii kushiriki katika harakati za kupinga upanuzi uliopo, au mpya, wa miradi ya mashamba makubwa ya miti.

Shamba kubwa la miti vamizi ya mikaratusi ikivunwa katika Jimbo la Mpumalanga, Afrika Kusini. Huu ni muonekano unaongezeka kuwa wa kawaida katika maeneo ya Afrika ambapo mashamba makubwa ya mikaratusi yanapandwa kwa ajili ya uzalishaji wa viwanda wa vifaa vitokanavyo na timbao ikiwa ni pamoja na mazao ya miti iliyosagwa na kuandaliwa kuwa kama uji ambao hutumika kuandaa karatasi (uji huo pia hujulikana kama massa), karatasi na vifungashio.

2. Taarifa za nyuma/usuli

Kutoka mwishoni mwa karne ya 19 mpaka katikati ya karne ya 20, wakati zikiwa chini ya udhibiti wa kisiasa wa Uingereza – koloni ambalo lilikuwa na nguzu zaidi kwa wakati huo - nchi nyingi za Afrika zilishinikizwa kuanzisha mashamba makubwa ya mbao kama suluhisho la iliyodhaniwa kumalizika kwa misitu yao. Mwaka 1876, Afrika Kusini ilikuwa miongoni mwa nchi za kwanza kuanzisha mashamba makubwa ya mikaratusi ili kutoa mafuta kwa ajili ya injini za garimoshi, na mashamba makubwa ya misindano kwa ajili ya mbao zilizotumika katika ujenzi[5,6], ikifuatiwa baadaye na Swaziland, Uganda na Kenya. Kuanzia mwaka 1945, baada ya mwisho wa Vita Kuu ya II, mashamba makubwa ya mbao yalipanuliwa ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa za timbao na vifaa ambavyo vilikuwa adimu katika nchi zilizoendelea kiviwanda, kwa kiasi fulani ni kutokana na ongezeko la matumizi ya kuni wakati wa vita ambazo zilihitajika kwa madhumuni ya kijeshi.

Kwa mujibu wa Jacovelli (2014)[7], kutoka miaka ya 1960 na kuendelea, mashamba makubwa ya miti zaidi yalianzishwa katika Afrika, yakisukumwa na idara za taifa za misitu ambazo pia zilifanya tafiti husika na mafunzo. Jinsi nchi zilivyopata uhuru kutoka kwa Uingereza katika miaka hiyo, zilipata msaada zaidi kutoka taasisi mbalimbali za maendeleo kwa ajili ya kuanzisha idara za 'misitu' pamoja na kuanzisha mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda. Mojawapo ilikuwa ni Shirika la Maendeleo la Koloni la Uingereza (CDC) (baadaye Jumuiya ya Madola), ambalo lilianzisha mashamba makubwa ya mbao pamoja na viwanda vya kuzalisha mazao ya miti iliyosagwa na kuandaliwa kuwa kama uji ambao hutumika kuandaa karatasi (uji huo pia hujulikana kama massa) na karatasi katika nchi kadhaa za Mashariki na Kusini mwa Afrika, ikiwemo Tanzania, Afrika Kusini na Swaziland. Mbali na Madagascar - koloni la zamani la Ufaransa - na Zimbabwe, ambayo ilisimamishwa mwaka 2002, nchi zote zilizoelezewa katika taarifa hii ni wanachama wa Jumuiya ya Madola.

Taasisi nyingine ya kimataifa inayosaidia mchakato wa upanuzi wa mashamba makubwa ya miti ni Benki ya Dunia, ambayo inafadhili mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda katika nchi za Kenya, Malawi, Tanzania na Swaziland, na pia katika Zambia kupitia CDC. Serikali ya Norway, kupitia shirika lake la maendeleo la NORAD, imefadhili mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda nchini Uganda na Tanzania, wakati serikali ya Ufini (Finland) imehamasisha upanuzi wa mashamba makubwa ya miti katika nchi za Msumbiji na Kenya.

Tangu miaka ya 1980, Shirika la Fedha Duniani (IMF)[8] liliegemea kwenye sera za mtindo wa uchumi wa kiliberali mamboleo na kupitishwa na benki za maendeleo kama Benki ya Dunia, zilitumika kulazimisha "mipango ya kurekebisha muundo" kwenye nchi nyingi za Kusini mwa dunia. Ili kupata fedha kutoka IMF za kulipa madeni kwa serikali za Kaskazini na mabenki, nchi zililazimika kuhamasisha ubinafsishaji, biashara huria, na kutoa motisha wa kuuza nje na ruzuku kwa makampuni - ikiwa ni pamoja na mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda.

Zaidi ya miaka 5 hadi 10 iliyopita, ubinafsishaji wa 'rasilimali' za kitaifa (ardhi inayomilikiwa na serikali na mashamba makubwa) umekuwa ukikamilika zaidi kupitia upatikanaji wa fedha kutoka benki za 'maendeleo' na mifuko ya uwekezaji ya binafsi na ya umma. Hii imeruhusu mashirika kupata ardhi inayomilikiwa na serikali na jamii kwa bei nafuu, na kufanya gharama nafuu za uwekezaji katika mashamba mapya na yaliyopo ya miti katika Afrika, kama sehemu pana ya mchakato wa uporaji wa ardhi na rasilimali asili.

Jukumu muhimu katika kuendesha upanuzi wa mashamba ya miti limekuwa likitekelezwa na Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) la Umoja wa Mataifa (UN) Kupitia taasisi za maendeleo za kimataifa kama vile CDC, Benki ya Dunia na mashirika ya misaada ya maendeleo kutoka nchi za Kaskazini, FAO imekuwa ikiwajibika kwa kuanzisha, na kukuza mfano wa mashamba makubwa ya 'misitu' ya Kaskazini kote Afrika. Mfano huu wa kiviwanda wenye mizizi ya Ulaya unaegemea kwenye ufafanuzi potofu ambao msitu unaonekana tu kama 'rundo' la miti lenye madhumuni ya msingi ya kuzalisha mbao[10].

---

[5] Overbeek W, Kröger M, Gerber J.F. 2012. An overview of industrial tree plantation conflicts in the global South. Conflicts, trends, and resistance struggles. EJOLT Report No. 3, p.100

[6] [7] Jacovelli, P.A. 2014, The future of plantations in Africa, International Forestry Review Vol16(2)

[8] The IMF was founded, together with the World Bank, during the Bretton Woods conference in 1944 in the USA, with the aim of rebuilding an international monetary system in the global North after World War II

[9] Overbeek W, Kröger M, Gerber J.F. 2012. An overview of industrial tree plantation conflicts in the global South. Conflicts, trends, and resistance struggles. EJOLT Report No. 3, p.100

[10] See http://wrm.org.uy/wp-content/uploads/2013/01/Definition_of_Forest.pdf ; and about industrial oil palm plantations expanding, but mainly in West and Central Africa (see http://wrm.org.uy/?s=oil+palm+in+africa)

FAO inadai kwamba mashamba makubwa ya kuzalisha mafuta ya mawese hayachukuliwi kama 'misitu, ispokuwa ni zao la kilimo, kwa sababu "yameanzishwa hasa kwa madhumuni mengine zaidi ya mbao".[11] Hii inaanika maslahi finyu ya FAO katika kukuza misitu na mashamba makubwa ya miti kama chanzo cha timbao badala ya kuchukua utaratibu wenye uwiano mzuri zaidi. Kwahiyo, ufafanuzi wa kupotosha ya FAO kuhusu 'msitu', ni pamoja kilimo cha zao moja lenye umri unaolingana, cha kiwango kikubwa kwa ajili ya viwanda, kawaida katika mashamba makubwa ya mamilioni ya miti vamizi isiyo ya asili pamoja na aina mbalimbali za mikaratusi na mierebi (poplar), iliyobadilishwa vinasaba ambayo imeelezewa kiupotoshaji kama "misitu ya kupandwa". Ufafanuzi huu wenye upendeleo unashindwa kutambua kazi nyingine muhimu na thamani halisi ya misitu, pia hupuuza majukumu muhimu ya jamii ambazo zimeishi kiuendelevu humo, zimelinda, na hutegemea misitu kwa ajili ya maisha yao na utambulisho wao wa kiutamaduni.

Ufafanuzi finyu unaolenga katika timbao/mbao/kiasi cha kaboni kilichopo kwenye mashamba makubwa ya miti na misitu ambayo kwa pamoja inaitwa "misitu", hata hivyo huwapa manufaa mengi, na faida ya fedha, kwa makampuni ya mashamba ya mbao na viwanda vinavyotumia timbao. Mashirika mengi ya Umoja wa Mataifa na wajumbe wa serikali kwa ujinga wanatumia dhana zinazopotosha za FAO za 'misitu,' upandaji miti 'na' upandaji tena wa miti 'kwa mashamba mkubwa ya miti, katika dhana ya uongo kwamba upandaji wa miti yoyote, hata kama ni aina ngeni vamizi, ni kujenga misitu. Ufafanuzi wa sasa wa FAO kuhusu msitu ni matokeo ya ushawishi mzito kwa baadhi ya serikali za wanachama wake kwa niaba ya maslahi ya mashirika. Hata hivyo, FAO imeshindwa kupanua fikra sawa na hizo kwa jamii tegemezi kwa misitu na watu wengine ambao maeneo yao yamevamiwa na mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda. Makundi haya hayajapewa nafasi ya haki ya kujumuishwa kikamilifu katika mchakato wa kimataifa wa kushauriana katika kuandaa fafanuzi sahihi na zenye kukubalika za mashamba makubwa ya miti na misitu.[12]

Kwa kutumia ushawishi wake mkubwa, FAO imeweza kuamuru aina ya mfano wa 'misitu' wa kutumika katika Afrika, na kwahiyo pia inatarajia kutoka kwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa Kusini mwa dunia kwamba wanapaswa kupitisha kanuni na fafanuzi za 'misitu kwa ajili ya viwanda' za FAO. Hili linathibitishwa na taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Sera ya Misitu ya Afrika Kusini ambayo inasisitiza kuwa Afrika Kusini ina nia ya kutumia istilahi na ufafanuzi wa FAO kwa sababu "... katika mjadala wa sera za kimataifa za misitu [... Kamati ya misitu ya FAO (COFO) na Jopo la Kimataifa la Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC)] mashamba makubwa yanakubaliwa na kutambuliwa kama misitu"[13]. FAO na ufafanuzi wake wa 'msitu' pia huwa na ushawishi wa maamuzi ya kisera na utendaji wa taasisi nyingine za kimataifa na kikanda na miundo inayohusiana na masuala ya misitu katika bara la Afrika. Hizi ni pamoja na Benki ya Dunia, Majadiliano ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), Mazungumzo ya Mkataba wa Bioanuai (CBD) ambayo mwenyeji wake ni Mradi wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Mazingira (UNEP), Kongamano la Umoja wa Mataifa kuhusu Misitu (UNFF) na kongamano la Misitu la Afrika (AFF).

Wakati wa kongamano la 14 la misitu la Dunia (WFC) lililofanyika mjini Durban mwezi Septemba mwaka 2015, (WFC ni mkutano mkuu wa kimataifa kuhusu misitu na elimu ya misitu unaoandaliwa na FAO kila baada ya miaka sita), Mpango mbadala[14] uliandaliwa na makundi ya asasi kadhaa za kiraia za Afrika Kusini na kimataifa ili kupinga sera ya FAO ya kukuza mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda. Katika siku moja wakati wa tukio hili, maelfu ya watu waliandamana katika mitaa ya Durban mpaka kwenye ukumbi wa mkutano huo ili kuieleza FAO kwamba mashamba makubwa ya miti si misitu. Watu walikuwa wakipinga dhidi ya jukumu la FAO katika kukuza upanuzi wa mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda kote barani Afrika na Kusini mwa dunia. Mwishoni mwa maandamano, pingamizi pamoja na saini zaidi ya 100,000 kutoka duniani kote, na kudai mabadiliko ya msingi katika ufafanuzi wa FAO, ili kukomesha uharibifu unaoendelea wa misitu na maeneo mengine yenye thamani kiikolojia kama vile savannahs na nyanda za nyasi na unaofanywa na mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda zilikabidhiwa kwa maafisa wa WFC na FAO.[15]

---

[11] http://www.fao.org/docrep/017/ap862e/ap862e00.pdf

[12] http://wrm.org.uy/wp-content/uploads/2013/01/Definition_of_Forest.pdf

[13] SA Department of Water Affairs and Forestry re 'Plantations are not Forests' debate. Forest Policy Directorate, 27-3-2001

[14] http://www.timberwatch.org/index.php?id=119

[15] http://wrm.org.uy/actions-and-campaigns/tell-the-united-nations-plantations-are-not-forests

Timu ya mdahalo ya FAO katika mjadala wa pili wa umma wa FAO dhidi ya Asasi za kiraia, uliofanyika mwishoni mwa programu za WFC na CSAP. Kulia-kushoto, Tiina Vahanen, Eduardo Mansur, Jeff Campbell.

Maelfu ya stika zilisambazwa kwa makundi wakati wa maandamano ya 'Matembezi ya Misitu Halisia' kupeleka pingamizi[16] wakiwa na zaidi ya saini 100,000 kwa waandaaji wa WFC

Bango la mpango mbadala wa asasi za kiraia (CSAP) ililotumika wakati wa matembezi ya Misitu halisia na kupinga 'misitu bandia' ambayo yalifanyika Durban, Afrika Kusini terehe 10 Septemba mwaka 2015.

16 https://www.rainforest-rescue.org/petitions/1013/tell-the-united-nations-plantations-are-crops-not-forests



Ramani (iliyofanyiwa marekebisho) inayoonyesha usambaaji wa aina kuu za uoto wa asili (biomes) katika mashariki na kusini mwa Afrika. Chanzo: Basic Maps of Africa[17]

Maeneo yanayolengwa kwa ajili ya upanuzi uliopo, au kwa uanzishwaji wa mashamba makubwa mapya ya miti katika mashariki na kusini mwa Afrika, kwa kawaida ni yale yenye hali bora ya ukuaji wa miti, hasa pale ambapo kuna mvua kati ya 800 na 1200mm kwa mwaka. Misitu ya mvua ya kitropiki, misitu ya pwani, na kanda za mapori ya savanna zilizoonyeshwa kwenye ramani ya kanda hapo juu kwa ujumla ni maeneo ambayo mashamba makubwa ya miti inayokua kwa haraka itafanya vizuri, kwasababu ni mahali ambapo itapata maji ya kutosha na aina za udongo unaofaa.

Makampuni ya mbao pia yanapendelea kupanga miradi ya mashamba makubwa katika maeneo yenye miundo mbinu kimkakati ndani ya kanda hizo na hali bora ya ukuaji wa miti, kwa mfano, kando ya barabara kuu, karibu na reli, vituo vya mijini na/au bandari. Maeneo ya ardhi inayofaa ambayo yamelengwa kwa ajili ya upanuzi wa mashamba makubwa ni, kutokana na sifa zao, pia ambapo wanajamii mara nyingi wanaweza kuendesha maisha yao, au ambapo ardhi inaweza kutumika kulima na kuvuna chakula kitakacho sambazwa kwenye masoko ya ndani. Pindi udongo wenye rutuba unapovuliwa bioanuai na udongo wa juu pia, na kuachwa na kiasi kidogo sana cha rutuba kwa matumizi au thamani ndogo kwa jamii; kupitia makampuni yasiyojali ya mbao, massa na karatasi yenye tamaa za muda mfupi ambayo hayaoni mbali zaidi ya faida. Matokeo yake ni uwezekano wa kutokea migogoro na wanajamii wakipinga uvamizi wa ardhi yao.



18

[17] Source: http://www.catsg.org/cheetah/07_map-centre/7_1_entire-range/basic-maps/africa_vegetation.gif

[18] Source: http://www.fao.org/docrep/u3500e/u3500e06.htm

3. Mashamba makubwa ya miti yaliyopo na ya baadaye

Chanzo kikuu cha taarifa rasmi kuhusu eneo la ardhi lililo chini ya mashamba makubwa ya miti katika nchi mbalimbali ni FAO. Hata hivyo, ili kukusanya ripoti zake za 'msitu', FAO hutegemea zaidi takwimu zilizotolewa na serikali za kitaifa. Uhakika wa takwimu zilizopo unategemea kama, au kwa kiwango gani cha usahihi nchi hukusanya takwimu zao za maeneo yaliyofunikwa na miti. Kama serikali haiwezi kutoa taarifa zinazohitajika, basi FAO inaweza kuteka habari kutoka vyanzo vingine kama vile taarifa za mbao za makampuni. Kwa sababu hizo na nyingine, takwimu za FAO si mara zote ni za kuaminika, na katika nchi kadhaa, watu wamedai kwamba eneo la shamba kubwa la miti kiuhalisia ni kubwa kuliko ilivyoelezwa katika takwimu rasmi za FAO.[19]

Jedwali la 10: Misitu ya kupandwa kati ya mwaka 1990 - 2015

Nchi/Himaya	Misitu ya kupandwa (1 000 ha)						Kiwango cha mabadiliko kwa mwaka							
	1990	2000	2005	2010	2015	Mwelekeo wa safu	1990–2000		2000–2010		2010–2015		1990–2015	
							1 000 ha/yr	%	1 000 ha/yr	%	1 000 ha/yr	%	1 000 ha/yr	%
Kenya	163	120	166	193	220	1	-4.3	-3.0	7.3	4.9	5.4	2.7	2.3	1.2
Lesotho	6	8	9	10	17	1	0.2	3.2	0.2	2.4	1.3	10.5	0.4	4.3
Madagascar	231	272	290	415	312	1	4.1	1.6	14.3	4.3	-20.6	-5.5	3.2	1.2
Malawi	132	197	285	365	419	1	6.5	4.1	16.8	6.4	10.8	2.8	11.5	4.7
Msumbiji	38	38	24	12	75	2	0.0	0.0	-2.6	-10.9	12.6	44.3	1.5	2.8
Afrika Kusini	1626	1724	1750	1763	1763	1	9.8	0.6	3.9	0.2	0.0	0.0	5.5	0.3
Swaziland	160	150	145	140	135	2	-1.0	-0.6	-1.0	-0.7	-1.0	-0.7	-1.0	-0.7
Uganda	34	32	31	55	60	1	-0.2	-0.6	2.3	5.6	1.0	1.8	1.0	2.3
Tanzania	150	200	230	240	290	1	5.0	2.9	4.0	1.8	10.0	3.9	5.6	2.7
Zambia	60	60	60	62	64	1	0.0	0.0	0.2	0.3	0.4	0.6	0.2	0.3
Zimbabwe	154	120	108	87	87	1	-3.4	-2.5	-3.3	-3.2	0.0	0.0	-2.7	-2.3

Jedwali: Eneo la "misitu ya kupandwa" (mashamba makubwa ya miti) kutoka mwaka 1990 – 2015 kwa nchi husika 11, kama ilivyonukuliwa kutoka kwenye jedwali la FAO "Tathmini ya Rasilimali za Misitu ya Dunia 2015"[20]

"Tathmini ya Rasilimali za Misitu Duniani" (FRA 2015), iliyotolewa Septemba 2015 katika Kongamano la Misitu la Dunia (WFC) nchini Afrika Kusini, ilipendelea kutumia "misitu ya kupandwa" kumaanisha mashamba ya miti. Hata hivyo, hapo awali ilishawahi kutumia maneno yenye utata na kupingana kama vile "msitu wa shamba", shamba la kibiashara", "shamba la msitu", "misitu", "upandaji upya wa miti" na "upandaji tena wa miti"[21] wakati ikimaanisha mashamba ya miti. Ripoti ya FAO ya mwaka 2016 kuhusu 'Hali ya Misitu ya Dunia'[22], hasa katika sehemu inayohusu Ghana (uk.70), inatumia maneno hayo bila mpangilio kabisa.

---

19 Overbeek W, Kröger M, Gerber J.F. 2012. An overview of industrial tree plantation conflicts in the global South. Conflicts, trends, and resistance struggles. EJOLT Report No. 3, p.100

20 GLOBAL FOREST RESOURCES ASSESSMENT 2015 Desk reference, FAO, 2015 - http://www.fao.org/3/a-i4808e.pdf

21 See FAO A & R definitions, 2000, Holmgren ftp://ftp.fao.org/docrep/fao/006/ad665e/ad665e00.pdf

22 See FAO 'State of the World's Forests 2016' - http://www.fao.org/3/a-i5588e.pdf

Kulingana na maelezo ya FAO, mwenendo wa jumla kati ya mwaka 1990 na 2015 katika nchi 11 zilizo chini ya wigo wa ripoti hii, isipokuwa Swaziland na Zimbabwe, ni mojawapo ya nchi zenye upanuzi wa mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda. Hata hivyo, kuna sababu ya kutilia shaka usahihi wa taarifa iliyotumiwa na FAO katika kufanya mahesabu ya mabadiliko ya maeneo yaliyofunikwa na misitu au mashamba makubwa ya miti kwasababu inaonekana kuwa baadhi ya nchi huenda zikawa na maeneo yanayochanganya pale ambapo mashamba makubwa ya miti au maeneo yaliyoingiliwa na miti ya kigeni imejiimarisha katika nafasi ya misitu ya asili na kuwa misitu. Peter Holmgren wa CIFOR amejaribu kutetea tofauti kubwa kati ya taarifa iliyopo katika ripoti ya FRA 2015 ya FAO, na takwimu kutoka katika satilaiti za Waangalizi wa Kimataifa wa maswala ya Misitu (Global Forest Watch) za ufuatiliaji wa mabadiliko katika eneo la ardhi lililofunikwa na misitu.[23] Peter Holmgren awali alikuwa ameajiriwa katika FAO, ambapo alisaidia kukuza dhana kwamba maeneo ya mashamba makubwa ya miti lazima yahesabiwe kama misitu wakati wa kuhesabu maeneo ya kimataifa yaliyofunikwa na misitu. Hii inaweza kuwa na maana kwamba eneo halisi la msitu ambalo limepotea limetolewa maelezo pungufu, wakati mashamba makubwa ya miti yasiyo rasmi na 'uvamizi wa miti ya mwituni' usiodhibitiwa unaweza kuwa unapanuka kwa kasi.

Nchi	1990	1995	Mabadiliko	2015	Mabadiliko	2035
Afrika Kusini	1626 000	1428 600	137 000	1763 000	177 000	1940 000
Swaziland	160 000	135 000	-25 000	135 000	5 000	140 000
Lesotho	6 000	6 000	11 000	17 000	13 000	30 000
Zambia	60 000	60 000	4 000	64 000	20 000	84 000
Zimbabwe	154 000	110 000	-67 000	87 000	13 000	100 000
Malawi	132 000	122 000	287 000	419 000	-269 000	150 000
Msumbiji	38 000	45 000	37 000	75 000	95 000	170 000
Kenya	163 000	240 000	57 000	220 000	80 000	300 000
Tanzania	150 000	200 000	140 000	290 000	50 000	340 000
Uganda	34 000	26 000	26 000	60 000	30 000	90 000
Madagascar	231 000	335 000	81 000	312 000	48 000	360 000
Total Jumla	2754 000	2707 600	688 000	3442 000	262 000	3704 000
Chanzo	FRA 2015	FAO[24]	FRA 2015	FRA 2015	Makadirio	Makadirio

Jedwali linalolinganisha makadirio ya zamani na ongezeko kati ya mwaka (1990-2015) na makadirio yanayoweza kutokea baadaye ya upanuzi au upunguzaji wa mashamba makubwa ya miti kati ya mwaka 2015 na 2035, kwa kuzingatia tathmini ya FRA ya mwaka 2015 (tazama hapo juu) na ripoti nyingine za FAO, kama vile kutoka kwenye tabiri nyingine zilizonukuliwa katika taarifa hii. (Angalizo: Istilahi zisizo sahihi, utoaji wa taarifa zisizowiana, uwezekano wa makosa ya kimahesabu, na ufafanuzi wenye utata wa FAO wa 'msitu', inaweza kuwa na mchango wa tofauti katika baadhi ya makadirio ya mwaka 1990/1995-2015 ya yanayoitwa maeneo ya "misitu ya kupandwa" hapo juu, kwa mfano ongezeko kubwa la eneo la Malawi la "misitu ya kupandwa". Makadirio kwa nchi kati ya 2015-2035 huenda yakawa ya kweli zaidi.)

Kama ilivyoonyeshwa katika jedwali hapo juu, kupata taarifa za kuaminika au sahihi kuhusu kiwango halisi cha mashamba makubwa ya miti inaweza kuwa changamoto, na hii inafanya makadirio ya baadaye kuwa magumu zaidi. Makala hii iliyopo kwenye blog ya Yona Busch inatoa ushahidi wenye nguvu katika kuunga mkono dai hili.[25]

---

23 http://blog.cifor.org/34669/can-we-trust-country-level-data-from-global-forest-assessments?fnl=en

24 FAO Forest Plantations Working Papers - *TROPICAL FOREST PLANTATION AREAS - 1995 DATA SET* - Based on the work in 1997 of D Pandey, May 2002 ftp://ftp.fao.org/docrep/fao/006/Y7204E/Y7204E00.pdf

25 http://www.cgdev.org/blog/three-reasons-fao%E2%80%99s-new-forest-numbers-don%E2%80%99t-add

Katika utafiti wa matumizi ya timbao katika Afrika, mfuko wa usimamizi wa uwekezaji uitwao Global Environmental Fund (GEF), - usichanganywe na ule Mfuko wa Mazingira wa Benki ya Dunia (pia unajulikana kama GEF) - unatarajia kuwa mahitaji ya timbao za viwandani na kuni katika Afrika yataongezeka kwa zaidi ya 70% katika kipindi cha mwaka 2010-2030.

Vile vile, mwaka 2012, kazi ya ushauri ya Indufor ya Ufini (Finland) ilitabiri kuongezeka kwa mahitaji ya timbao, na wastani wa upanuzi wa mashamba makubwa ya miti katika Afrika wa hekta 40,000 mpaka 50,000 kwa mwaka. Indufor inaona takwimu hizi kuwa za chini ikilinganishwa na kanda nyingine, kutokana na ugumu wa kuanzisha miradi mipya ya kupanda miti katika Afrika. Ingawa inaamini kuna "maeneo makubwa ya ardhi, yenye rutuba ambayo hayajaendelezwa yenye kufaa" kuwa mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda, inaashiria kwamba hakuna mtaji binafsi wa kutosha utakaowekezwa kwa sababu ya hatari kubwa ya migogoro na wanajamii ambao wanadai umiliki wa ardhi iliyolengwa kwa ajili ya mashamba makubwa[26].

Tathmini ya Indufor kuwa Afrika ina uwezo mkubwa wa kuanzisha mashamba mapya ya miti umethibitishwa na watendaji wengine kadhaa, kama vile Benki ya Dunia na taasisi za fedha za kimataifa, ikiwa ni pamoja na mifuko ya pensheni ambayo ni miongoni mwa wale wanaowekeza humo, na kukuza upanuzi wa mashamba makubwa ya miti katika mashariki na kusini mwa Afrika. Shirika la ushauri la Indufor pia lenyewe lina "miradi ya shambani" nchini Zambia, Tanzania, Msumbiji na Afrika Kusini.[27]

Uvamizi wa miti ya 'Mwituni' kama kichaka hiki cha mikaratusi ya 'gundi ya mwituni' nchini Afrika Kusini, inaweza ikafuzu kuwa 'misitu' kulingana na sheria ya FAO, lakini kiuhakika haipaswi kuitwa hivyo. Wala haipaswi kuwekwa kwenye kundi la mashamba ya miti, ambayo yana haja ya kuandikishwa kama 'watumiaji maji, na kupata leseni kwa ajili ya matumizi yao ya maji na kupunguza mtiririko wa mkondo, ili iweze kuwa "halali", katika suala la Sheria ya Taifa ya Maji ya Afrika Kusini (No.36 wa 1998).

26 www.globalenvironmentfund.com/wp-content/uploads/2013/05/GEF_Africa-will-Import-not-Export-Wood1.pdf

27 http://pubdocs.worldbank.org/pubdocs/publicdoc/2016/3/509791457041122238/Indufor-forestry-investments.pdf

4. Wanaoendesha upanuzi wa mashamba ya miti

Upanuzi wa mashamba makubwa ya miti kama njia ya uporaji wa ardhi Afrika

Kwa mujibu wa Jacovelli (2014), mwendeshaji mkuu wa wimbi jipya la miradi ya mashamba makubwa ya miti katika Afrika katika kipindi cha miaka 5 -10 ni mtaji wa fedha uliolenga ulanguzi wa muda mrefu katika ardhi chini ya mashamba makubwa ya miti kama chaguo la uwekezaji mpya. Wengi wa wawekezaji hawa wangependa baadhi mashamba makubwa yaliyokomaa yajumuishwe, ili kupokea marejesho ya mapema kwenye uwekezaji wao. Wawekezaji wa aina hiyo ni pamoja na benki zote mbili maendeleo - Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) na Benki ya Dunia pamoja na kampuni yake tanzu ya kibiashara na mwanachama wa kundi la Benki ya Dunia, Shirika la Kimataifa la Fedha (IFC), pamoja na taasisi binafsi kama vile benki za biashara, mifuko ya pensheni, na kile kinachoitwa 'mfuko wa uwekezaji wa kijani', kwa kutumia fedha kutoka vyanzo binafsi na vya umma.

Wimbi hili la wawekezaji kuja katika Afrika linaweza kutazamwa kama sehemu ya mchakato mpana wa uporaji wa ardhi unaofanyika katika mataifa ya Kusini, lakini ambao unailenga Afrika hasa ili kupata ardhi yenye uzalishaji kwa gharama ya chini sana. Lengo lao kuu ni kuanzisha miradi mikubwa ya kukuza mbao, sukari, na mazao mengine ya kilimo kwa kuuza nje kwa nchi za walaji. Hata hivyo, ardhi pia inalengwa kwa ajili ya shughuli nyingine za viwanda kama vile madini na ranchi binafsi za wanyama kwa ajili ya utalii. Katika mashariki na kusini mwa Afrika, hili wimbi jipya la uporaji wa ardhi ya kigeni umeleta mipango kama vile ProSavana kaskazini mwa Msumbiji.[28] Ili kuwezesha uporaji wa ardhi na makampuni yao wenyewe, nchi za mataifa ya Kaskazini zimetengeneza sheria mpya za fedha zilizoundwa kufanya uwekezaji katika nchi za kigeni na katika uanzishwaji wa miundombinu kuwa rahisi zaidi. Kwa mfano, mwaka 2004 serikali ya Marekani ilianzisha Shirika la Changamoto za Milenia (MCC), ambalo lina jukumu muhimu katika kubidhaifisha mashamba ya Afrika na kuyafungua kwa mashirika ya Marekani ambayo msingi wake ni kilimo. MCC ina miradi katika mashariki na kusini mwa Afrika, kwa mfano katika Madagascar na Msumbiji.[29] Taasisi kama IMF, Benki ya Dunia na benki nyingine za maendeleo hutunga sera zao zenye mwelekeo huo.

Katika nchi nyingi za Afrika, kuna ardhi ambayo rasmi ni mali ya serikali lakini kiuhalisia inamilikiwa na wanajamii ambao wamekuwa wakiishi humo kwa vizazi vingi. Namna ambavyo imekuwa ikitumika ilipangwa kupitia sheria za kimila na mamlaka za jadi za jumuiya hizo. Katika nchi nyingi, jamii, wenyeji na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanayosaidia yamekuwa yakishiriki katika harakati za pamoja ili kupata utambuzi rasmi wa kimila, umiliki wa pamoja wa ardhi inayotumika na kumilikiwa na jamii.

Kwasababu hiyo haswa, ni kipaumbele kwa taasisi za wafadhili wa kigeni, kama vile MCC, ili kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa manufaa ya makampuni ya kigeni na wawekezaji wao. Kwa MCC, Haki za ardhi za kimila zinaonekana kama kikwazo kwa lengo lao la kuwa na udhibiti salama juu ya maeneo ya ardhi ambayo wangependa kuona yako katika mikono ya wawekezaji. Kwa mujibu wa Jolyne Sanjak wa MCC: "Kile ambacho sisi tunafanya na serikali ni kuhakikisha kwamba mikataba ya kukodisha ardhi ni salama, kwamba mchakato wa kumalizika muda wa kukodisha na kuhamisha ukodishaji ni wa ufanisi". Matokeo yake, uwezekano wa kupata mikataba salama ya kukodisha imeendesha wawekezaji wengi kuomba umiliki wa ardhi. Nchini Msumbiji kwa mfano, hekta milioni kadhaa za ardhi nzuri zaidi zimeangukia katika mikono ya makampuni na wawekezaji katika miaka ya hivi karibuni, ikiwa ni pamoja kwa ajili ya kupanda mashamba makubwa ya miti.[30] Hata hivyo, suala siyo tu kuhusu upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya mashamba ya miti. Makampuni ya mbao ya kigeni na wawekezaji katika miradi ya mashamba makubwa ya miti na kilimo cha biashara kwa uwazi wanataka kupata si tu ardhi yoyote, lakini kupata ardhi katika Afrika yenye uwezo bora wa kilimo. Markus Grulke, mkurugenzi mtendaji wa kampuni ya usimamizi wa mashamba ya kipekee, ambayo imeshirikiana na kampuni ya uwekezaji wa kilimo katika hatua ya kujenga Mfuko wa (uwekezaji) Arbaro, hivi karibuni alisema: "sisi tunaangalia uwekezaji ambapo ukuaji wa hali ya juu wa miti ya mbao kwa hekta unaweza kupatikana. Katika nchi za tropiki (hari) kikwazo ni mvua na hali ya udongo. Tunaenda tu katika kanda ambazo zina mvua za mwaka zinazofikia 1,200mm".

---

28 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section2/prosavana-plan-in-mozambique-is-out-and-threatening-peasants- land

29 https://www.grain.org/article/entries/4501-the-great-food-robbery-a-new-book-from-grain

30 https://www.grain.org/article/entries/4501-the-great-food-robbery-a-new-book-from-grain

Wakati serikali zinapowezesha upatikanaji wa ardhi yenye rutuba kwa kuikodisha kwa wawekezaji au kuingia nao makubaliano, wanawapa msamaha wa hitajio la wao kuwekeza sehemu ya fedha zao katika kununua ardhi, na hii huwatia moyo wa kumiliki ardhi zaidi ambayo kutokana na hiyo wanaweza kuongeza faida zaidi. Kwa mujibu wa Grulke, "Tumejifunza katika miaka [hivi karibuni] kwamba [mifano ya ardhi ya kukodisha] pia ni chanya na yenye faida. Tumekuwa na uzoefu mzuri sana katika mifano ya ardhi ya kukodisha ... Kwa ukodishaji unaweza ukapata ardhi kubwa ambayo si kwa ajili ya kuuza. Hii ina maana kwamba utengenezaji wa thamani ya kiuchumi na athari ni wa juu sana kwasababu unapanda eneo kubwa kwa kiasi hicho hicho cha fedha. Kukabiliana kwako na hewa ya ukaa na uzalishaji wa mbao pia ni wa juu kwa mtaji ule ule wa uwekezaji "[31].

Mfuko wa Arbaro uliotajwa hapo mwanzoni, una lengo la kupata jumla ya kiasi cha Euro milioni 200, tayari ushapata EUR milioni 50 kutoka katika Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, na wana mipango ya kuwekeza katika mashamba ya miti katika Afrika na Amerika ya Kusini.

---

31 https://www.agriinvestor.com/12595-2/

Mfuko wa dunia wa mshikamano wa misitu: Utengenezaji wa faida au kutokomeza umasikini?

Miongoni mwa wawekezaji wapya katika miradi ya mashamba makubwa ya miti barani Afrika ni baadhi ya watendaji ambao kihistoria wamekuwa na jukumu kubwa katika shughuli mbalimbali kuhusu kazi za misaada na kutokomeza umaskini, si katika shughuli za biashara binafsi: Makanisa. Mfano Mfuko wa Dunia wa Mshikamano wa Misitu (GSFF), uliopo Sweden ambao uliundwa na Dayosisi ya Vasteras, Kanisa la Kilutheri la Sweden, na ushiriki wa mfuko wa Kanisa la Kilutheri la Norway. Hata hivyo, mwekezaji mkuu mwenye (57%) ya milioni 100 za Marekani zilikuwa siyo za kanisa bali za Mfuko wa Pensheni wa Uholanzi, ABP. (1)

GSFF ilishirikiana na Kanisa la Anglikana katika jimbo la Niassa nchini Msumbiji, kampuni inayomilikiwa na Harvard ya Diversified International Timber Holdings LLC, na Mfuko wa Misitu wa Denmark, katika kampuni ya mashamba makubwa ya miti ya Chikweti, katika Niassa. Askofu wa Anglikana wa Niassa alikuwa mwenyekiti wa kampuni kwa kipindi hicho. (2)

Chikweti ilikuza mashamba yake ya miti ya aina moja kuwa ni yenye manufaa kijamii, lakini badala ya kusifiwa kwa kutokomeza umaskini, kampuni hiyo ilishutumiwa kwa athari kwenye jamii za wakulima wadogo wadogo wa ndani. (3) Labda kwasababu ya hali hii, GSFF ilihamishia mali zake zote za Msumbiji kwa kampuni inayomilikiwa na Green Resources (GR) ya Norway mwaka 2014, na GR kuchukua mashamba ya miti ambayo hapo awali yemekuwa yakisimamiwa na Chikweti.

Kumbuka: Ilikuja baadaye kuripotiwa kwamba Green Resources ilikuwa ikikabiliwa na "mtiririko hasi wa fedha", na kwahiyo Mfuko wa Uwekezaji wa Phaunos uliamua kuuza 14% ya hisa zake zenye "hatari kubwa" katika Green Resources. (4) Ripoti ya vyombo vya habari: " Kampuni ya misitu ya Norway inapata hasara kubwa baada ya ununuzi wa kampuni yake ya Msumbiji" (5) inafunua mengi kuhusu hali ya kifedha ya Green Resources.

---

(1) www.fian.org/fileadmin/media/publications/PR_-_2012.10.16_-_Tree_plantations_Niassa_Mozambique.pdf
(2) https://www.svenskakyrkan.se/default.aspx?id=1139326
(3) www.wrm.org.uy/oldsite/bulletin/161/Mozambique.html
(4) www.phaunostimber.com/content/uploads/2014/04/PHAUNOS-Annual-Report-Dec-2015-FINAL-PRINTED.pdf
(5) http://zitamar.com/norwegian-forestry-firms-losses-mount-mozambique-acquisitions

Baadhi ya watendaji wakuu katika upanuzi wa mashamba makubwa ya miti

Ufafanuzi wa makusudi wenye utata wa FAO kuhusu msitu, na takwimu zake zinazopotosha za "eneo la ardhi lililofunikwa na misitu", hufanya FAO kuwa mhusika, lakini pia kuwa mchangiaji asiyewajibika katika mchanganyiko wa waendeshaji wenye utata na ukaidi ambao wako nyuma ya mipango ya upanuzi wa mashamba makubwa ya miti katika mashariki na kusini mwa Afrika.

Kwa mfano, utaratibu wa kufafanua mashamba ya miti kama "aina ya msitu" inaficha kiwango halisi cha uharibifu wa misitu ya kitaifa na kimataifa. Pia husaidia kutuliza nchi ambazo kamwe hazijawahi kuwa na misitu, au tayari zimepoteza misitu yao yote, kwasababu inaruhusu wao kudai kwamba wanatengeneza au kuongeza "eneo la ardhi lililofunikwa na misitu". Chini ya "Mkataba wa Paris" uliopitishwa hivi karibuni, ambao sasa ndiyo majibu rasmi ya Umoja wa Mataifa ya kukabiliana na mgogoro wa tabianchi[32], mashamba makubwa ya miti pia yanaainishwa kama "misitu" yenye uwezo wa muda mfupi wa kuhifadhi hewa ukaa iliyofyonzwa kutoka angani. Hii hutoa motisha wa kutengeneza zaidi "eneo la ardhi lililofunikwa na misitu" na mashamba ya miti, ambayo pia kimakosa huitwa "misitu ya kupandwa" katika lugha isiyoeleweka ya FAO. Lakini hii ni kukuza ufumbuzi wa uongo kwenye mgogoro wa tabianchi, ambao utasababisha matatizo mengi mapya kwa jamii barani Afrika, ikiwa ni pamoja na uharibifu wa mazingira ya asili, wakati mashamba makubwa ya miti yanapovamia maeneo yao.[33]

Kundi jingine muhimu la watendaji ambalo linakuza na kuwa na maslahi ya moja kwa moja ya fedha katika upanuzi wa mashamba makubwa ya miti kimataifa, ni washauri wataalamu wa kimataifa wa 'misitu', hasa kutoka katika nchi za mataifa ya Kaskazini ambazo zina viwanda vilivyoanzishwa vya timbao kama vile Ufini (Finland), Sweden, Ujerumani, na Marekani. Indufor na Pöyry kutoka Finland, kwa mfano, yanasaidia kutambua 'masoko mapya' na 'kusaidia' serikali za kitaifa katika kuandaa 'mipango ya msitu' ambayo mara nyingi inatilia mkazo zaidi juu ya mashamba makubwa mapya ya miti[34].

Kwa mfano, mwaka 2011 Pöyry ilitoa "Tathmini ya mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda katika Afrika", ambayo ni kwa ajili ya kuuza kwa wanunuzi wenye nia kwa karibia dola za Marekani 11,000. Ripoti hii inaonyesha "ni nchi zipi zina uwezo mzuri kwa ajili ya maendeleo ya upanuzi wa mashamba makubwa" na pia "ni nchi zipi kwa sasa ni 'muhimu' kwa ajili ya maendeleo ya mashamba makubwa". Pamoja na kwamba itakuwa gharama kubwa kupata maelezo, utangulizi uliochapishwa kwenye mtandao unaonyesha madhumuni matatu muhimu ya mashamba makubwa ambayo wawekezaji wanaweza kuchunguza kama wana mpango wa kuwekeza katika Afrika:

- "Uwezo mzuri wa kuendeleza masoko ya ndani kwa bidhaa za timbao";
- Mtazamo wa Pöyry wa Afrika kama "chanzo muhimu cha baadaye cha tungamotaka kwa ajili ya sekta ya nishati hai ya Ulaya";
- Na tathmini ya Pöyry ya Afrika kama "sehemu mwafaka kwa ajili ya kusambaza magogo na timbao zinazofaa kutengeneza massa katika masoko ya Asia".

Kuiunga mkono ripoti ya Pöyry kutawezesha upatikanaji wa habari juu ya "motisha/ruzuku ambao unaweza kupatikana kwa waendelezaji wa mashamba makubwa" katika nchi zilizochaguliwa. Nchi zote za mashariki na kusini mwa Afrika zilizojadiliwa katika taarifa hii zimeelezewa kwa ufupi katika utafiti wa Pöyry kama nchi zenye fursa za uendelezaji wa mashamba makubwa ya miti[35].

Mashirika na/au wizara za ushirikiano wa maendeleo ya serikali za nchi hizo za Kaskazini kama makampuni ya ushauri yaliyotajwa kabla, ikiwa ni pamoja na Finnfund (Finland), NORAD (Norway), SIDA (Sweden) na DIFID (Denmark) mara nyingi pia yanafanya kazi ya kusaidia nchi kuweka 'mazingira mazuri ya ndani' kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya miti. Kwa mfano, katika Tanzania programu ya Ufini inayofadhiliwa na serikali hiyo ilizinduliwa mwaka 2013 ili kukuza uwekezaji wa sekta binafsi katika miradi ya kupanda miti katika nchi.[36] Hata hivyo, miaka mitatu tu baadaye, shughuli hii imetambuliwa kuwa haifai, yenye uwezekano wa kusababisha matatizo ambayo yanahitaji kufanyiwa tathmini mara moja[37].

---

32 Because it is based on the belief that the climate crisis is just an issue of too much carbon in the wrong place: the atmosphere (see also in http://wrm.org.uy/actions-and-campaigns/the-climate-and-forest-crises-cannot-be-solved-with-number-games-and-false-solutions)

33 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section1/new-forests-for-africa-a-nice-slogan-for-promoting-industrial-tree- plantations

34 Overbeek W, Kröger M, Gerber J.F. 2012. An overview of industrial tree plantation conflicts in the global South. Conflicts, trends, and resistance struggles. EJOLT Report No. 3, p.100

35 http://www.poyry.com/sites/default/files/africanplantationforestry - june2011-lfwp-br.pdf

36 Jacovelli, P.A. 2014. The future of plantations in Africa. International Forestry Review Vol16(2)

37 http://drp.dfcentre.com/project/timber-rush-private-forestry-village-land

Sababu za ukuzaji wa miradi ya mashamba makubwa ya miti

Ripoti ya hivi karibuni[38] juu ya maendeleo ya mashamba ya miti kimataifa, ilitoa mazingatio juu ya mwenendo wa kuanzisha mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda kwa matumizi mbalimbali, kwa lengo la fursa mpya na nyongeza, pengine kama njia ya kukabiliana na madhara ya mtikisiko wa kiuchumi duniani. Ili kubaki katika mwenendo huu, mradi wa shamba kubwa la miti unaweza kutumika katika kuzalisha ongezeko la gesi ya ukaa na pia kwa ajili ya kuuza kwa wachafuzi wa mazingira wa Kaskazini [39], pamoja na kuzalisha mbao kwa ajili ya kuuza katika masoko ya ndani. Vinginevyo, timbao kutoka kwenye mashamba makubwa zinaweza kutumika kwa ajili ya uzalishaji wa massa, au kuuza nje katika nchi za Ulaya kama timbao tungamotaka kwa uzalishaji wa nishati. Sambamba na hali hii, wawekezaji katika miradi ya mashamba makubwa ya miti wa mashariki na kusini mwa Afrika mara nyingi hutaja kusudi au bidhaa zaidi ya moja ili kukuza mashamba yao, na hivyo kuwa na matumaini ya kupanua chaguzi za kuongeza faida zitokanazo na miradi yao.

Mashamba makubwa kwa ajili ya mbao (magogo) au nishati (kuni/mkaa)

Kwa mujibu wa utafiti wa kampuni ya uwekezaji ya Marekani ya mwaka 2013, Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF)[40], "kuna vipengele vikuu viwili kwa matumizi ya timbao katika Afrika: kuni na nguzo kwa ajili ya viwanda". Inakadiria jumla ya matumizi ya kila mwaka ya timbao katika Afrika kuwa karibu milioni 700m^3, ambazo milioni 75m^3 hutumika kwa ajili ya bidhaa za viwandani, na salio (milioni 625m^3) huunguzwa kama kuni au mkaa, zaidi kuliko katika bara jingine lolote. Aidha, kwa mujibu wa GEF, matumizi yote yanaweza kuongezeka katika siku za usoni. Kwa sasa, nyingi ya timbao zinazotumiwa zinatokana na uoto wa asili wa timbao, ikiwa ni pamoja na misitu.

Wawekezaji kadhaa katika miradi ya mashamba makubwa ya miti katika nchi za mashariki na kusini mwa Afrika wanasema kuwa mashamba yao yatasambaza magogo kwa ajili ya samani au mbao kwa ajili ya kuni, kwa masoko yote ya ndani na nje. Hii ni kwa mujibu wa kampuni ya Green Resources (GR) inayomilikiwa na Wanorway, ambayo ina mashamba ya miti na vinu vya kuchana mbao katika Tanzania, 'mashamba makubwa ya miti ya kufidia/sawazisha hewa ukaa' nchini Uganda, na pia wanadai kuhusika na uzalishaji wa mkaa nchini Msumbiji[41].

Makampuni kama vile GR yote yanashinikiza uwepo wa mashamba makubwa ya mikaratusi na misindano, mara nyingi hudai kwamba shughuli zao hupunguza shinikizo kwenye misitu ya asili. Hata hivyo, mara nyingi zaidi kinyume chake ndiyo ukweli. Nchini Msumbiji, baada ya karibu miaka 10 ya uwekezaji katika upanuzi wa mashamba makubwa ya mikaratusi na misindano, misitu ya asili imendelea kuharibiwa kwa ajili ya uvunaji na uuzaji nje wa mbao zenye thamani ya juu kutoka aina nyingine zisizokuwa za mikaratusi au misindano. Mara nyingi mbao huvunwa na kuuzwa nje kinyume cha sheria nchini China.[42] Kwa upande mwingine, upanuzi wa mashamba makubwa ya miti umekuwa ukishutumiwa kama sababu za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja za ukataji wa miti. Kwa mfano, kwa mujibu wa jamii zilizoathirika, upanuzi wa mashamba ya miti katika jimbo la Niassa Msumbiji umeharibu maeneo makubwa ya misitu. Mwanakijiji wa jamii ya Micoco katika Niassa, akimaanisha Chikweti, moja ya makampuni makuu yaliyokuwa yakifanya kazi katika ukanda huo, alisema: " Wanaangusha miti na kila kitu kilichopo juu ya ardhi yetu" .[43]

38 https://www.tni.org/en/collection/flex-crops

39 For information on carbon credit projects in Africa, see http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section1/uganda-carbon-plantations-generate-benefits-for-foreign-investors-and-certifiers-while-communities-pay-price-of-displaced-livelihoods

40 www.globalenvironmentfund.com/wp-content/uploads/2013/05/GEF_Africa-will-Import-not-Export-Wood1.pdf

41 http://www.greenresources.no

42 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/forests-in-mozambique-face-extinction

43 http://wrm.org.uy/books-and-briefings/an-overview-of-industrial-tree-plantations-in-the-global-south-conflicts-trends-and-resistance-struggles

Mashamba ya uzalishaji massa na karatasi

Timbao ni malighafi kuu inayotumika katika uzalishaji wa karatasi. Kama yalivyo mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda yalivyopanuka kwa haraka zaidi katika Kusini mwa dunia kuliko katika Kaskazini kwa zaidi ya miongo miwili iliyopita, ndivyo hivyo viwanda vinavyochafua vya massa na karatasi vimefuata mwenendo huo. Mashirika makubwa ya kimataifa ya massa na karatasi yamefunga viwanda vyao ambavyo ni vya ghali na chakavu huko Kaskazini, na kujenga vipya na vikubwa zaidi huko Kusini. Hata hivyo, viwanda hivi vipya vya massa huuza nje zaidi ya uzalishaji wao kwenye kanda zenye viwanda vingi ambapo matumizi ya mtaji ni ya juu zaidi, k.v. nchi katika mataifa ya kaskazini. Mfano halisi ni viwanda vya massa vya Sappi ya SAICCOR na Ngodwana vya Afrika Kusini ambavyo hubadilisha timbao kutoka mashamba makubwa ya miti na kuzalisha zaidi ya tani milioni ya "kemikali ya cellulose" (huvunja kamba kamba za massa) kila mwaka kwa ajili ya kuuza nje. China inaagiza toka nje massa nyingi zaidi katika miaka ya hivi karibuni, ingawa sehemu yake ni kwa ajili ya kusambaza kwa idadi inayoongezeka ya watu wake wa mijini. Hata hivyo, sehemu kubwa ya ongezeko la matumizi ya massa na karatasi katika China ni kutokana na mahitaji ya ufungaji kutoka sekta yake ya viwanda, kufungashia bidhaa kwa ajili ya kuuza nje, kama vile kuzalisha bidhaa za kufanyia usafi na vitambaa vya viscose (ambavyo ni mchanganyiko unaopatikana kwa kuyeyusha massa kwa kutumia kemikali) kwa sekta ya nguo, tena kwa kiasi kikubwa ili kukidhi mahitaji kutoka kwa wateja katika mataifa ya Kaskazini.

Lakini mwenendo wa kuenea na kupanua mashamba na viwanda vipya vya massa katika mataifa ya Kusini bado haujashamiri katika mashariki na kusini mwa Afrika, mbali na Afrika Kusini. Vimelundikana zaidi katika Amerika ya Kusini na Asia. Kati ya nchi 11 ndani ya wigo wa ripoti hii, ni nchi 4 tu ndizo zenye viwanda vya massa, vingi asili yake vikiwa vilijengwa wakati wa katikati ya miaka ya 1900. Afrika Kusini ina viwanda 10 vya massa, vingi vikiwa vinamilikiwa na makampuni ya kimataifa ya Sappi na Mondi. Kiwanda cha Sappi ya Usutu katika Swaziland kilijengwa karibia miaka 65 iliyopita, lakini kilisimama kufanya kazi mwaka 2010 na kuuzwa mwaka 2014.[44] Kenya ina kiwanda kimoja tu cha massa na karatasi, sehemu ya kundi la Pan African Paper Mills (PPM) na sehemu inayomilikiwa na serikali ya Kenya (33.4%), Orient Paper Company ya India (24%) na Benki ya Dunia IFC (29%). Kuna kiwanda kimoja tu kidogo cha karatasi katika Tanzania, Mufindi Pulp and Paper, ambacho awali kilianzishwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia wa dola za Marekani milioni 60 mwaka 1986, na kisha kuuzwa mwaka 2004 kwa Rai Group kutoka Kenya kwa dola za Marekani million 1 tu.[45]

Sababu moja ya hali hii ni kwamba viwanda vipya vya massa vinahitaji hekta 50,000 hadi 100,000 za mashamba ya miti karibu na kiwanda ili kuhakikisha usambazaji unaoendelea wa kutosha wa 'magogo safi'. Kwa mujibu wa utafiti wa GEF[46] uliotajwa kabla, karibia 64% ya mashamba ya miti katika Afrika yanachukuliwa kuwa na ubora hafifu au wa kawaida, na si yenye uzalishaji wa juu. Aidha, ujenzi wa viwanda vipya vya massa - ambavyo daima huwa ni vikubwa zaidi kuliko vile vya zamani - unahitaji uwekezaji mkubwa wa bilioni kadhaa za dola za Marekani, ambayo ni gharama zaidi kuliko ile ya kuanzisha mashamba makubwa ya miti. Hii pia inahitaji kuwa kampuni inapata dhamana kutoka serikali ya nchi zinazohusika kabla ya kuamua kwenda mbele na uwekezaji mkubwa kama huo. Dhamana kwa kawaida hutoa motisha wa fedha na ruzuku, vifaa vya kwa ajili ya kuagiza mitambo na kuuza bidhaa, pamoja na miundombinu mizuri (barabara na vifaa vya bandari), ambavyo ni nchi chache barani Afrika zinaweza kutoa.

Mbali na kukabiliwa na vikwazo vilivyotajwa hapo juu, kiwanda kipya cha massa katika Afrika kingetakiwa pia kushindana na vile ambavyo tayari vimeshaanzishwa na kuimarika katika nchi nyingine za Kusini, kama vile Brazil na Chile katika Amerika ya Kusini, na Indonesia na China katika Asia, ambapo makampuni yanayoungwa mkono na serikali za kitaifa pia yana nia ya kuongeza uwezo wao wa uzalishaji. Viwanda vilivyopo mara nyingi viliundwa kwa njia ambayo inawezesha upanuzi baadaye katika eneo moja.

Sababu nyingine ambayo inafanya kuwa vigumu kwa miradi ya viwanda vya massa kuanza kupanua mashamba makubwa katika ukanda huu, ni kwamba tangu mtikisiko wa kiuchumi wa mwaka 2008 nchini Marekani na Ulaya, mahitaji ya massa na karatasi yamepungua, na hivyo kuathiri vibaya mipango mipya ya uwekezaji.[47]

---

44 http://www.observer.org.sz/news/64036-swazis-buy-usutu-forest-for-e1-billion.htm

45 http://www.lesprom.com/en/news/Tanzanias_Mufindi_Paper_Mills_in_full_production_35141

46 http://www.globalenvironmentfund.com/wp-content/uploads/2013/05/GEF_Africa-will-Import-not-Export-Wood1.pdf

47 http://www.cepi.org/taxonomy/term/26

Lakini hii haina maana kwamba Afrika haitalengwa na upanuzi zaidi wa eneo la mashamba yake makubwa ya timbao kwajili ya massa. Inaweza ikawa vizuri sana, kwa mfano, kusambazia viwanda vya massa katika sehemu nyingine, na kusafirisha nje vibanzi vya timbao (wood chips). Makampuni katika Chile awali yaliuza nje vibanzi hivyo kwa ajili ya uzalishaji massa katika nchi nyingine, kabla ya kujenga kiwanda chao cha kwanza cha massa. Siku hizi, sehemu ya uzalishaji wa mbao ya Afrika Kusini inauzwa pia nje katika mfumo wa vibanzi, hasa kwa Japan, ambayo ina kiwanda kikubwa cha karatasi na ufungashaji lakini wana misitu au mashamba ya miti machache kutokana na eneo lake dogo la ardhi.

Kwa sasa, inaonekana kwamba kuna kiwanda kimoja tu kipya cha massa kilichopangwa kujengwa katika mashariki na kusini mwa Afrika, mradi unaoungwa mkono na Benki ya Dunia (IFC) nchini Msumbiji (tazama maelezo ya nchi) cha kampuni ya Kireno ya Portucel. Mradi huo bado upo katika awamu ya kwanza ya kujaribu kuanzisha mashamba makubwa ya miti, na kama kiwanda hicho kitajengwa, kinatarajiwa kuanza uzalishaji ifikapo mwaka 2025[48]. Hata hivyo, inatarajiwa kwamba Green Resources watajaribu kupata fedha kwa ajili ya kiwanda chake cha massa nchini Msumbiji, vinginevyo watajaribu kuunganisha nguvu pamoja kampuni nyingine ya ndani yenye mashamba makubwa. Inasema katika tovuti yake: "Green Resources inaamini Nacala ni eneo zuri sana kwa ajili ya kiwanda cha massa hapo baadaye na inatarajia uzalishaji mkubwa wa vibanzi vya timbao na/au nishati itokanayo na mgandamizo wa vumbi la mbao (wood pellets) kuanza vizuri kabla ya kiwanda chake cha massa."[49]

Hata hivyo, kampuni ya ndani ya Justiça Ambiental - Ja! (Friends of the Earth Msumbiji) inapinga mipango ya Portucel kwa ajili ya kiwanda cha massa, na hivi karibuni ilitoa ripoti iliyopewa kichwa cha **"Portucel – Mchakato wa upatikanaji wa ardhi na haki za jamii"**. Kuipata ripoti hii ya kireno *"Portucel - O Processo de acesso à Terra e os direitos das comunidades"* nenda https://issuu.com/justicaambiental/docs/portucell_com_graficos_novos_

Bwawa ambalo halijadhibitiwa (lisilo na uzio na ulinzi) la maji taka yaliyochafuliwa, na nyuma kuna mashamba makubwa ya mikaratusi kwa ajili ya kuzalisha timbao zilizosagwa kwa ajili ya kutengeneza karatasi. Hii ni katika Mpact (zamani Mondi Packaging)[50] Kiwanda cha kutengeneza massa na karatasi (FSC-C117980) karibu na mji wa Piet retief jimbo la Mpumalanga, Afrika Kusini.

48 http://en.portucelmocambique.com/Portucel-Mocambique

49 http://www.greenresources.no/Plantations/Mozambique/Lurio.aspx

50 http://www.bdlive.co.za/business/industrials/2016/05/24/mpacts-profit-warning-sends-share-plunging

Mashamba makubwa ya miti kama hifadhi ya hewa ukaa inayotolewa

Wazo la kuanzisha maeneo ya 'hewa ukaa inayohifadhiwa ' imekuwa ikiendesha upanuzi wa mashamba makubwa ya miti katika Mashariki na Kusini mwa Afrika kwa zaidi ya miongo miwili, katika kuitikia fursa ya kutengeneza fedha kiurahisi kwa kuzalisha na kuuza kinachojulikana ongezeko la kaboni. Upandaji wa miti umejumuishwa kama vile aina mojawapo ya kukabiliana mabadiliko ya tabia nchi chini ya Mfumo wa Maendeleo Safi (CDM) wa Itifaki ya Kyoto, kama ilivyokubaliwa mwaka 1997 chini ya Mkakati wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC). Hii ilikuwa eti ni kusaidia kukabiliana na mgogoro wa mabadiliko ya tabianchi, lakini ilikuwa hasa ni nia ya kusaidia kukidhi maslahi ya nchi za Kaskazini na makampuni ambayo hayakupendelea kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa (CO_2) kwenye viwanda vyao. Walichagua badala yake kuwekeza katika kinachojulikana "mfumo wa maendeleo safi" (pia inajulikana kama 'ufumbuzi wa uongo tabianchi'), kama vile kupanda kiasi kikubwa cha miti katika nchi za Kusini mwa dunia. Ni wazi kabisa kuwa, hii ilionekana kama mbadala nafuu sana wa kupunguza uzalishaji wa CO_2 nyumbani kwao.

Mbali na hilo, makampuni ambayo yamewekeza katika miradi hiyo pengine pia yalitarajiwa kuboresha taswira kwa umma kutokana shughuli 'chanya' na 'kijani' ya kupanda miti katika Afrika. Hata hivyo, matokeo yamekuwa kinyume tu: Kwa mfano, mwaka 1994 mojawapo ya miradi ya kwanza ya mashamba makubwa ya miti ya kukabiliana na hewa ukaa ilianzishwa nchini Uganda na shirika la FACE la Uholanzi (sasa linaitwa Face the Future). Ukiwa umefunika hekta 25,000 za ardhi katika kingo za mbuga za Mlima Elgon, mradi huu ulisababisha ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Wenyeji walifukuzwa katika eneo hilo na walipoteza shughuli za kuendesha maisha yao; na mradi huo ulishutumiwa kama aina ya ukoloni mamboleo.[51]

Licha ya ukiukwaji wa masuala ya kijamii na kimazingira na 'waanzilishi wa mradi' huu, miradi kama hii ya mashamba makubwa ya hewa ukaa iliendelea kuanzisha katika Uganda na nchi nyingine za Afrika katika kipindi cha miaka iliyofuata. Mifano ni kampuni ya Uingereza ijulikanayo kama New Forests Company, pia katika Uganda[52], pamoja na kampuni iliyotajwa kabla ya Green Resources ya Norway (GR) [53], ambayo kwa msaada wa fedha kutoka serikali ya Norway (Norfund) na IFC, ilianzisha maelfu ya hekta za mashamba duni ya miti kwenye ardhi ya jamii katika kusini mwa Tanzania, na kisha ilijigamba kwenye tovuti yake kwamba ni "moja ya makampuni ya kwanza duniani kupokea mapato ya hewa ukaa kutoka katika mashamba yake makubwa ya misitu "[54]

Hadi sasa, masoko ya hewa ukaa yamekuwa ni anguko la kifedha, na matokeo yake ni bei za ongezeko la hewa ukaa zimebaki kuwa chini. Upanuzi wa aina hii ya mashamba makubwa ya miti umekuwa wa kasi ndogo zaidi kuliko mapromota wao walivyotegemea. Kasi ndogo ya ukuaji wa miradi hii kwa kiasi kikubwa ni kutokana na ukiukwaji wa haki za binadamu katika ngazi ya jamii kuwa wazi kwa umma; ambao unaonyesha umuhimu wa kujulikana kwa migogoro hiyo.[55] Ukiukwaji wa haki za watu kwa uwazi unaonyesha kwamba kilichokuwa cha umuhimu zaidi kwa wamiliki wa miradi hiyo ni miti na kaboni iliyohifadhiwa katika timbao zao, si ardhi au wanajamii walioathirika. Kinyume chake, wanajamii walioathirika mara nyingi wanaonekana kama tishio la kufikia malengo ya mradi.

Ripoti iliyochapishwa na Timberwatch mwaka 2011 inaelezea athari hasi za kijamii na kimazingira za mradi wa shamba kubwa la miti la hewa ya ukaa iliyohifadhiwa wa Green Resources 'katika Idete kusini mwa Tanzania.[56] Kwa kuzingatia hili, na namna ambavyo Green Resources imeweza kupanua kwa kasi shughuli zake zenye utata za mashamba makubwa ya miti katika nchi kadhaa za kusini mwa jangwa la Sahara, pia inaibua maswali muhimu kuhusu nia ya kweli ya wawekezaji wake wa kitaasisi, kwa mfano Norfund[57].

---

51 http://wrm.org.uy/wp-content/uploads/2013/02/Place_Store_Carbon.pdf

52 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section2/uganda-new-forests-company-fsc-legitimizes-the-eviction-of-thousands-of-people-from-their-land-and-the-sale-of-carbon-credits

53 http://carbonmarketwatch.org/engos-and-scientists-challenge-the-swedish-energy-agency-stop-supporting-false-climate-change-solutions-in-uganda/

54 http://www.greenresources.no/News/tabid/93/articleType/ArticleView/articleId/3/Green-Resources-First-CDM-Registration-in-Uganda-and-Tanzanian-VCS-Sales-Agreement.aspx

55 http://www.pambazuka.org/governance/unclean-development-mechanism

56 http://timberwatch.org/uploads/TW%20Tanzania%20CDM%20plantations%20report%20low%20res%20(1).pdf

57 http://www.norfund.no/eastern-africa/green-resources-article342-319.html

Mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya biodizeli au mafuta yatokanayo na tungamotaka za timbao

Mwaka 2009, Umoja wa Ulaya (EU) uliamua kwamba nchi wanachama zinapaswa kuzingatia 20% ya lengo la nishati mbadala la mwaka 2020. Kati ya mwaka 2006 na 2010, mashamba makubwa ya mibono (*Jatropha curcas*) yalikuwa ni miongoni mwa mashamba makubwa ya kwanza ya nishati hai (bioenergy) kuanzishwa katika kanda ili kukabiliana na kwa kutarajia mahitaji ya mafuta ya dizeli yatokanayo na mimea katika EU. Mashamba makubwa ya Jatropha yalianzishwa nchini Tanzania, Msumbiji, Madagascar na Swaziland ili kuzalisha biodizeli kutoka katika mbegu za jatropha[58]. Hata hivyo, karibu miradi yote hii imeshindwa, na mwishowe, ruzuku kutoka EU ilinufaisha wale tu ambao walipokea fedha moja kwa moja, kama vile waandaaji wa mradi na washauri wataalamu.

Nyingi ya nishati mbadala za 'kijani' zinazohitajika katika EU zinatarajiwa kutokana na kuunguza tungamotaka za timbao. Ulaya haina miti ya kutosha iliyopandwa katika eneo la ardhi yake yenyewe ili kukidhi mahitaji hayo, hivyo sasa inaagiza kiasi kikubwa kinachooengezeka cha tungamotaka za timbao, nyingi kutoka kusini mwa Marekani, ambayo bado ina maeneo makubwa ya misitu na mashamba makubwa ya miti. Hii ina maana kwamba hadi sasa mahitaji yanayoongezeka ya tungamotaka za timbao kutoka baadhi ya nchi za EU bado na haijawa na nguvu kubwa ya kuendesha upanuzi wa mashamba makubwa ya miti katika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Hata hivyo, Afrika bado inaweza kuwa ni muuzaji nje mwenye uwezo wa tungamotaka za timbao kwa Ulaya kama mahitaji yataongezeka, na rasilimali za Amerika ya Kaskazini za tungamotaka za miti zitakwisha. Kwa mara nyingine tena, Brazil na kanda na nchi nyingine ambazo zimejiimarisha zaidi katika kuzalisha mbao zina uwezekano mkubwa wa kuzishinda nchi za Afrika kwa soko la tungamotaka katika Ulaya. Labda nchi za pwani katika mashariki na kusini mwa Afrika ambazo kwa kiasi fulani ziko karibu na China na eneo la Asia ukilinganisha na Amerika ya Kusini zitakuwa na faida ya kiushindani kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya baadaye kutoka Asia.

Tishio la misitu ya Afrika na mipango ya upandaji tena wa miti

'Mkataba wa Paris' uliojadiliwa December 2015 huko Ufaransa ulifungua mlango wa fumbuzi kadhaa za uongo za mgogoro wa mabadiliko ya tabianchi. Miongoni mwa hizi ni utaratibu uliotajwa kabla wa kujaribu kuhifadhi kwa muda hewa ukaa kwenye miti, kwa kuweka miradi ya mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda. Wakati huo huo, nchi zenye viwanda vingi zinaweza kuongeza kutoa gesi ya ukaa na gesi nyingine chafu kwa kuchoma fueli za asili, (fossil fuels) huku ikizidisha mabadiliko ya tabianchi kwa muda fulani. Dhana ya 'kupanda tena miti' duniani, na hasa katika bara la Afrika, kwa mamilioni ya miti, ilipata nafasi maarufu katika baadhi ya matukio sambamba katika mkutano wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya tabia nchi. Ilisemwa kuwa Afrika ingekuwa na "fursa kubwa ya kurejesha misitu kuliko bara jingine lolote"[59].

Mpango kabambe wa 'upandaji tena wa miti' uliotangazwa Paris ulikuwa ni Mkakati wa Urejeshaji wa Mazingira ya Misitu ya Afrika (AFR100), ambao unapaswa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na juu yake uwe wa manufaa kwa watu wa Afrika. Mpango huu unadai kwamba hekta milioni 100 za 'misitu iliyokatwa ovyo' na ardhi 'iliyoharibiwa' katika Afrika inaweza kurejeshwa ifikapo mwaka 2030. Mpango huu una lengo la kusaidia (1) Changamoto ya Bonn (Bonn Challenge), ambao ni mkakati wenye dhamira ya kurejesha hekta milioni 150 duniani kote ifikapo mwaka 2020; (2) Azimio la New York la Misitu, ambalo linatilia mkazo na kupanua Mkakati wa Changamoto ya Bonn wa kurejesha hekta milioni 350 ifikapo mwaka 2030; na (3) Mkakati wa Kuimarisha Mandhari ya Afrika (Arli), ili kukuza usimamizi shirikishi wa mazingira kwa lengo la kurekebisha na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi[60].

Tangu miaka ya 1960, Benki ya Dunia imekuwa ikihamasisha kikamilifu mashamba makubwa mapya ya miti katika Mashariki na Kusini mwa Afrika na kimataifa, na ni mfadhili mkubwa na mmoja wa watetezi wakuu wa kimataifa wa mipango ya "upandaji tena wa miti". Benki ilitangaza kuwa itatoa kwa AFR100 kiasi cha dola za kimarekani bilioni 1 katika uwekezaji wa kitaasisi katika nchi 14 ifikapo mwaka 2030. Hii itakuwa inasaidiwa na Wizara ya Shirikisho la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (BMZ) ya Ujerumani ambayo itatoa msaada wa kifedha kwa mpango wa kujenga muundo wa AFR100.

58 http://www.recommon.org/eng/land-grabs-madagascar-voices-ground-2013-report-launch

59 http://www.wri.org/our-work/project/AFR100/about-afr100

60 http://www.wri.org/our-work/project/AFR100/about-afr100

FAO pia ni mmoja wa washirika muhimu katika mradi huo, kama vile Taasisi ya Rasilimali za Dunia (WRI). Wafadhili binafsi hasa ni makampuni ya uwekezaji wa mtaji kama vile Kampuni ya Kidachi ya Uwekezaji Endelevu wa Misitu (SFI)[61]. Jumla ya kiasi kilichoahidiwa na wafadhili binafsi kitakaribia dola za Marekani million 540[62]. Hadi sasa, ahadi kutoka serikali za Kiafrika katika suala la maeneo yanayotegemewa "kurejeshwa" na mpango inafikia jumla ya hekta milioni 41 katika nchi 13, ikiwa ni pamoja na zile kadhaa zilizo kwenye wigo wa taarifa hii: Kenya, Madagascar, Msumbiji, Malawi na Uganda.

Benki ya Dunia na FAO, pamoja na washirika wengine wa AFR100, pia waliongoza mpango wenye tamaa sawa na ule wa AFR100 zaidi ya miaka 30 iliyopita. Ulikuwa unaitwa Mpango Kazi wa Misitu ya Kitropiki (TFAP)[63]. TFAP nayo pia ilishindwa, na moja ya sababu ilikuwa ni pingamizi kali kutoka kwa jamii katika kujibu shinikizo la nguvu la TFAP la mashamba makubwa ya miti ya aina moja. AFR100, yenye watendaji walewale waliohusika, na walioandaa malengo yanayofanana na yale ya TFAP, kuna hatari kwamba itakuwa ni motisha mkubwa mwingine wa upanuzi wa kiwango kikubwa cha mashamba ya miti kwa ajili ya viwanda kama njia ya kufikia malengo yake ya 'marejesho katika hali yake ya asili'. Kwa mara nyingine tena, itakuwa ni kwa faida ya wawekezaji na makampuni ya mashamba makubwa ya miti, na kuleta matatizo mengi na ukiukwaji wa haki za binadamu kwa jamii.

Mwezi Aprili 2016, katika namna hiyo hiyo, Benki ya Dunia ilizindua Mpango Kazi wake wa Misitu (FAP) wa mwaka 2016-2020 ambao ulilenga kile kinachoitwa " misitu endelevu " na "Hatua Nadhifu za kuboresha Misitu" zijulikanazo kama *Forest smart interventions*. FAP ni mwongozo wa mipango mingine ya Benki ya Dunia inayohusiana na msitu kama vile Programu yake ya Misitu (PROFOR)[64] na Mpango wa Uwekezaji wa Misitu (FIP)[65]**.** Inasema kuwa "kimataifa, karibia hekta bilioni 2 ya ardhi ya misitu iliyoharibika ingeweza kurejeshwa kuwa mfumo wa mazingira unaofanya kazi, unaozalisha, ambao utasaidia kupambana na mabadiliko ya tabianchi". Mbali zaidi, ni wito kwa "kuongeza uwekezaji katika misitu ya kupandwa". Hii inatoa mwanga jinsi Benki ya Dunia inavyouona mfumo wa mazingira "unaofanya kazi" na "unaozalisha". Na kisha inasema kwamba ina lengo la "kufanya kazi kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kuwezesha modeli (mifano) zao za biashara kuwa misitu nadhifu", na baadaye kuongeza kwamba tawi la kibiashara la Bank, ambalo ni Shirika la Kimataifa la Fedha (IFC), "linaweza kushirikiana na sekta binafsi ya wawekezaji wanaowajibika…", kuhamasisha zaidi ya kile kinachoitwa" uwekezaji unaowajibika katika kiwango kikubwa cha upandaji tena wa miti ya kibiashara ".[88]

Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ukaa kutokana na ukataji miti na uharibifu wa Misitu (MKUHUMI) na Mfuko wa Kijani wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF)

Mwaka 2015 katika mazungumzo ya UNFCCC COP21 ya mabadiliko ya tabianchi yaliyofanyika mjini Paris, nchi ziliwasilisha kwa umma Michango ya Nchi zao katika Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (INDC), wakionyesha malengo ya kupunguza gesi chafu kuwa kila nchi kwa hiari ingejituma kuyafikia katika kipindi cha baada ya mwaka 2020. Msumbiji ilirejea katika INDC[67] yake ya mkakati wa MKUHUMI wa kitaifa kama njia ya kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa kupitisha ufafanuzi ya msitu katika mkakati wao wa kitaifa wa MKUHUMI[68] ambao uko sawa na, kwa kuzingatia ufafanuzi wa FAO kuhusu misitu wa 'kipimo kimoja kinatosha wote', mkakati wa MKUHUMI wa kitaifa wa Msumbiji unafungua mlango wa "misitu ya kupandwa" - soma mashamba makubwa ya miti ya kupandwa ya aina moja – kwa ajili ya kufyonza kaboni, kama fursa ya kuvutia fedha za mabadliko ya tabianchi. Kwa mfano, kupitia Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi, mmoja wa wafadhili wakuu, ulioanzishwa na serikali, fedha zitakuwa zinapatikana kufadhili shughuli za kukabiliana na mabadiliko.[69]

---

61 http://www.wri.org/our-work/project/AFR100/impact-investors#project-tabs

62 http://www.cp-africa.com/2015/12/07/10-african-couce-the-afr-100

63 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section1/tropical-forestry-action-plan30-the-fao-and-the-world-bank-are-at- the-center-of-another-false-solution-to-the-forest-crisis-redd-and-climate-smart-agriculture

64 www.profor.info

65 https://www-cif.climateinvestmentfunds.org/fund/forest-investment-program

66 http://documents.worldbank.org/curated/pt/2016/04/26229494/forest-action-plan-fy1620

67 http://www4.unfccc.int/submissions/INDC/Published%20Documents/Mozambique/1/MOZ_INDC_Final_Version.pdf

68 http://www.redd.org.mz/uploads/Relat%C3%B3rios/25.pdf

69 http://www.ciel.org/green-climate-fund-dos-and-donts-the-case-of-redd

'No REDD in Afrika Network (NRAN)[70] ni kundi la mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na watu binafsi wenye wasiwasi ambao wanaofanya kazi ya kufichua hali halisi ya makali ya MKUHUMI katika namna ambayo itasababisha madhara kwa jamii na uharibifu wa mfumo wa mazingira ya ndani bila kufanya chochote ili kuzuia mabadiliko ya tabianchi. Wao wanaamini kuwa MKUHUMI, kama ulivyo Mfumo wa Maendeleo Safi "upandaji upya wa miti na upandaji tena wa miti" ni ufumbuzi feki/bandia

Uthibitishaji kama motisha wa ukaidi kwa ajili ya upanuzi wa mashamba makubwa ya miti

Motisha mkuu kwa ajili ya makampuni ya mbao yaweze kuthibitishwa ni kwamba wawekezaji 'wawajibikaji' katika miradi ya mashamba makubwa ya miti kawaida wanahitaji cheti cha 'kijani' ili kuhakikisha 'ubora' wa uwekezaji kwa madhumuni ya masoko. Hapo ndipo wawekezaji wa aina hiyo watakuwa tayari kuweka fedha katika miradi ya mashamba makubwa kwasababu uthibitishaji huo hutoa aina ya 'ushahidi' kwamba uwekezaji ni 'mzuri'.

Ingawa ukaguzi wa uthibitisho unafanyika na mamlaka ya tatu ambayo inatakiwa kuwa huru inayojulikana kama 'bodi ya uthibitishaji, kampuni iliyoajiriwa kufanya ukaguzi na kuthibitisha mashamba hulipwa moja kwa moja na kampuni ya mashamba makubwa inayotafuta uthibitisho, ambayo inaibua maswali kuhusu uadilifu wa bodi za uthibitishaji zilizopitishwa na FSC. Uzoefu wa kinachojulikana kama "uthibitishaji wa msitu" katika kanda umeonyesha kuwa zoezi la kuthibitisha misitu au mashamba ya miti ('misitu feki') kama "misitu iliyosimamiwa kiuwajibikaji" na Baraza la Usimamizi Misitu (FSC), siku zote limefanya kazi ya kuhalalisha athari hasi za mashamba ya miti yaliyopo, na kuhalalisha kuanzishwa kwa mashamba makubwa mapya ya miti[71]. Mashamba makubwa mapya ya miti huwaondoa wanajamii au wanyamapori, huharibu mashamba au makazi ya asili, na kumaliza kabisa rasilimali za udongo na maji zinazohitajika ili kuendeleza vizazi vijavyo vya wakulima na watu wanaoishi mijini.[72] FSC imethibitisha karibia hekta zipatazo milioni 14 za mashamba hayo duniani kote.[73]

Mbali na kupitisha ubadilishaji unaoharibifu mazingira ya asili, mashamba yaliyolimwa na malisho ya mifugo, uthibitishaji wa mashamba makubwa ya miti unaofanywa na FSC pia unahalalisha 'mbinu za usimamizi' ambazo hutumiwa kwa makusudi ili kudhuru au kuharibu mimea ya asili na viumbe. Kwa mfano, baada ya kuwa miti imepandwa, viuatilifu vyenye sumu hutumiwa ili kutokomeza bioanuai tajiri ya mimea ya asili ambayo inaweza kushindana na mashamba makubwa ya miti kwa maji na virutubisho. Hii pia huanika/huacha wazi udongo na kuweza kusababisha mmomonyoko na kupotea kwa hewa ukaa ya kibiolojia. Dawa za kemikali pia hutumika katika kudhibiti wadudu na panya ambao wanaweza kula miti michanga baada ya chakula chao cha asili kutiwa sumu. Lakini mbaya zaidi ni mauaji ya wanyama wakubwa kama vile nyani, ambao wanatokomezwa kwa risasi, kutegwa au kuwekewa vyambo vyenye sumu. Nchini Afrika Kusini na Zimbabwe, maelfu ya nyani werevu sana, ambao wana mahusino ya karibu na binadamu, wamekuwa wakiuawa na makampuni ya mashamba makubwa ya miti. Licha ya upinzani kuhusu tabia hii, na malalamiko kuwasilishwa kwa FSC International na Asasi ya Kiraia ya Afrika Kusini ya GeaSphere[74], lakini bado mauaji yameendelea.[75]

Uchunguzi kifani (case studies) na makala zinazoelezea madhara ya uthibitishaji yamekuwa yakichapishwa, lakini baadhi ya NGOs kubwa za 'hifadhi' bado zinashirikiana na FSC na makampuni ya mbao katika kukuza mashamba ya miti ambayo yanasababisha madhara kwa viumbe hai na wanajamii. Mfano wa hili ni ushirikiano kati ya WWF na Mondi katika kuhimiza uanzishwaji wa kina wa kinachojulikana kama "Kizazi Kipya cha Mashamba Makubwa" (NGP), ambacho kweli siyo bora kuliko wastani wa mashamba makubwa ya miti yaliyopo katika Afrika Kusini, ambayo ni vigumu kukubalika.[76] Badala ya kujaribu kushughulikia athari hasi za mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda, uthibitishaji unaofanywa na FSC na miradi inayofanana imekuwa ni kampeni ya kutia kasumba ya kijani (greenwashing) katika kutangaza mashamba yao ya mbao na kuhamasisha bidhaa zake kuwa "ni sahihi katika mazingira, zenye manufaa kijamii, na zenye faida kiuchumi" . Hii imeruhusu sekta ya mashamba makubwa ya miti kupata kibali na msaada kutoka kwa serikali za kitaifa na mashirika ya Umoja wa Mataifa kama vile UNFCCC, FAO na Benki ya Dunia.

---

70 See the NRAN website for more information: www.no-redd-africa.org

71 https://fsc-watch.com

72 www.globalforestcoalition.org/wp-content/uploads/2010/11/LIFEASCOMMERCE-CERTIFICATION.pdf

73 http://wrm.org.uy/wp-content/uploads/2013/09/FSC_consultation_and_complaints_procedures.pdf

74 https://www.facebook.com/GeaSphere

75 http://thegreentimes.co.za/eco-label-allows-killing-of-wild-baboons

76 www.mondigroup.com/PortalData/1/Resources/newsroom/NGP_Media_Release_170614.pdf

5. Harakati za jamii dhidi ya mashamba makubwa ya miti

Ingawa wanaoendesha upanuzi wa mashamba makubwa ya miti barani Afrika na malengo tofauti ambayo mashamba makubwa hutumika yanaweza kuwa mengi, lakini athari kwa jamii mara nyingi zinafanana sana, kwa kuwa makampuni mengi hutumia modeli/mfano mmoja wa kiwango kikubwa cha uzalishaji, mara nyingi yakiwa ni mashamba makubwa ya mikaratusi, na pia mara kadhaa hutumia mikakati na mbinu zinazofanana za kukuza miradi yao katika mashariki na kusini mwa Afrika.

Kupoteza ardhi na vipato, na matokeo yake kwenye uhuru wa chakula

Moja ya changamoto kubwa kwa jamii katika kanda iliyo ndani ya wigo wa ripoti hii ni - katika muktadha wa mchakato mpana wa uporaji ardhi- ni kupata na kudumisha udhibiti wa ardhi ambayo wao hutegemea, na huitumia kulingana na mambo ya kimila. Hii ni kweli hasa katika Afrika mashariki ambapo karibia 75% ya wakazi wanaishi katika maeneo ya vijijini[77]. Mara nyingi, maisha yao ni tegemezi kwa chakula ambacho wao wenyewe wana uwezo wa kuzalisha.

Pamoja na kuwa serikali za kitaifa zinawezesha upatikanaji wa ardhi yenye rutuba kwa makampuni yenye mashamba makubwa na mitaji ya fedha, madhara katika maisha ya watu yanaweza kuwa ya haraka na majanga, ambayo yatapelekea jamii nzima kuondolewa katika makazi yao. Kulingana na ripoti ya Oxfam ya Septemba 2011, "Kampuni Mpya ya Misitu na mashamba yake makubwa ya Uganda", Mamlaka ya Taifa ya Misitu ya Uganda (NFA) ilitoa leseni ya umiliki kwa Kampuni Mpya ya Misitu (NFC) mwaka 2005 na kisha kuanza kuondoa wenyeji, ambao ilidai walikuwa 'Wavamizi haramu'. Jambo hili lilifanyika Februari 2010 katika Mubende na kati ya mwaka 2006 na Julai 2010 katika Kiboga. Utafiti wa Oxfam unakadiria kuwa idadi ya wanaopaswa kuhama ilikuwa 22,500, pamoja na kwamba takwimu zinaweza kuwa kubwa zaidi.[78]

Katika hali ambapo kiuhalisia makampuni hayakufukuza familia kutoka katika majumba yao, mara nyingi huzuia upatikanaji wa ardhi yao ya kilimo na misitu, na bado hukana kwamba hii inatokea. Katika jimbo la Nampula nchini Msumbiji, kwa mfano, makampuni kama vile Green Resources, yanafanya kazi chini ya jina la Lurio Green Resources, na kudai hadharani kwamba wao hupanda miti ya mikaratusi tu katika "nyanda za nyasi zenye thamani ya chini au ardhi ya misitu iliyoharibika." Hata hivyo wanakijiji ambao wameathirika moja kwa moja wanathibitisha kwamba kampuni inapanda kwenye ardhi ya kilimo, ardhi ambayo familia zilikuwa au zinatumia kwa ajili ya kuzalisha chakula chao, au zina mipango ya kutumia kama mashamba, yanayoitwa 'machambas'. Watu wanasema kuwa katika miaka ya hivi karibuni, wakati mashamba makubwa ya mikaratusi yalipoanzishwa kwenye ardhi ya jamii na kampuni hiyo, uzalishaji wa ndani wa chakula ulipungua[79].

Mbinu moja ambayo makampuni hutumia ili kuwezesha upatikanaji wa "machambas", ni kutoa ajira. Katika wilaya ya jimbo la Zambezia nchini Msumbiji, wanakijiji katika eneo ambapo kampuni ya kutengeneza massa na karatasi ya Portucel inakuza mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda - ITPs[80], walipatiwa ajira na kampuni kwa ajili ya kubadilishana na 'machamba' yao. Wanakijiji wanaripoti kwamba kampuni ilikuwa tayari kulipa karibia dola za Marekani 60 kwa mwezi. Lakini kazi ilikuwa tu kusafisha 'machamba' yao wenyewe, kuandaa ardhi kwa ajili ya kupanda miche ya mikaratusi, na baada ya kupanda, kuitunza miche hiyo katika awamu ya awali ya ukuaji. Baada ya hapo, wanakijiji walitoa taarifa kwamba kampuni iliwaachisha kazi, ingawa wao walitarajia kazi ingekuwa ya kudumu. Matokeo yake, walibakia 'ndani ya uzio' wa mashamba makubwa ya mikaratusi, bila kazi au ardhi ambayo kwayo huzalisha chakula chao.

Mwanakijiji katika jimbo la Nampula alishiriki katika mpango wa kukuza uzalishaji wa maharage ya soya. Lakini Lurio Green Resources ilitoa tu mbegu za awali, na baadaye kuchukua ziada ya 20% kutoka kwa wakulima. Kwa mfano, wale ambao walipata kilo 20 za mbegu za maharage walitakiwa kurejesha kilo 24 kwa kampuni baada ya mavuno. Mwanakijiji alieleza kwamba hakuna mtu katika jamii yao anayekula soya, kwa sababu si sehemu ya mlo wao wa jadi.

---

77 http://www.geohive.com/earth/pop_urban.aspx

78 www.oxfam.org/sites/www.oxfam.org/files/cs-new-forest-company-uganda-plantations-220911-en.pdf

79 Notes from a field trip by WRM to Mozambique in collaboration with Justiça Ambiental, 2015

80 Part of their plan to set up 60,000 ha of eucalyptus plantations - authorized by the Mozambique government, http://ifcextapps.ifc.org/ifcext/spiwebsite1.nsf/78e3b305216fcdba85257a8b0075079d/641968a1f67cea1185257d6200735d53?opendocument

Badala yake, soya zinazozalishwa huuzwa kwa sekta ya kuku. Hata hivyo, mkulima huyu alivunjika moyo kwasababu kipato chake kimekuwa kikipungua kutokana na bei ya soya kushuka kwa kiasi kikubwa tangu kuanza kwa mradi. Wakati huo huo, Green Resources haikuwa ni yenye kutoa msaada wowote wa kutafuta soko la mazao yake.

Upungufu wa maji uliosababishwa na mashamba makubwa ya miti

Changamoto nyingine kwa jamii ambazo zimefanikiwa kupinga kuondolewa, na kubaki katika majumba yao baada ya ardhi yao kuvamiwa na mashamba ya miti, ni kwamba kwa wakati fulani watateseka kutokana na uhaba mkubwa wa maji. Kwa kawaida hii hutokea baada ya miaka michache kwa vile mashamba yanazidi kuwa makubwa na kutumia maji zaidi, hasa wakati wa kiangazi. Ukame unaoendelea katika kanda ya kusini mwa Afrika umechochea athari zaidi za mashamba makubwa ya miti kwa rasilimali maji za juu na chini ya ardhi. Mbinu zinazotumiwa na makampuni ya kutuliza jamii zilizoathirika ni, kwa mfano, kutoa ahadi ya kuwapa visima.

Madhara mengine makubwa ambayo kwa asili yanahusishwa na modeli/mfano wa kiwango kikubwa cha mashamba ya aina moja ya miti kwa ajili ya viwanda ni athari za matumizi ya kemikali sumu za kilimo. Hii ni pamoja na sumu za kuulia magugu na wadudu, ambazo hutumika kuzuia ushindani wa ukuaji wa mimea au kuua mchwa na wadudu wengine au kuvu (fungi) ambao wanaweza kudhuru miti. Sumu hizo ni tishio kubwa kwa afya za wafanyakazi ambao huzitumia, hata kama wanatumia mavazi ya kinga, ingawa mara nyingi haifanyiki hivyo. Zinaweza pia kudhuru wanyama pori na mifugo ambayo hunywa maji yenye vimelea kutoka mito na maeneo yanayozunguka mashamba makubwa wa ajili ya viwanda, pamoja na wana jamii ambao pia hutumia maji machafu kutoka kwenye visima kwa ajili ya kufulia, kunywa na kupikia.



Mchoro unaoelezea athari za mashamba makubwa ya mikaratusi kwa maji ya chini ya ardhi kwa kulinganisha na uoto wa asili wa karibu (Chanzo: Brites, C.M. na Vermeulen, D. Athari ya mazingira ya chini ya ardhi katika eneo oevu la St. Lucia) [81]

81 http://gwd.org.za/sites/gwd.org.za/files/02%20C%20Brites_Environmental%20Impacts%20of%20the%20groundwater%20on%20the%20St.%20Lucia%20Wetland_Article_2013.pdf

Mojawapo ya nchi ambapo watu wameteseka zaidi kutokana na kumalizika kwa rasilimali ya maji ni Afrika Kusini. Ushahidi wa Bi Ziqubu kutoka kijiji cha Sabokwe unaeleza hali ya kawaida katika jamii ambazo ni majirani wa ITPs:

"Ukweli ni kwamba tunashindania maji na mashamba hayo. Wao hutumia maji mengi. Nakumbuka wakati tulipofika hapa mwaka 1996; mkondo wa karibu na bustani yetu ulikuwa unatiririka mwaka mzima kwasababu miti aina ya mikaratusi haikuwepo hapa. Kipande hiki cha ardhi kutoka hapa mpaka barabarani kilikuwa ni nyanda ya nyasi. Kampuni iliogopa tungepanda mazao na kujenga nyumba zetu juu yake hivyo kwa haraka walipanda miti katika ardhi hiyo. Tangu wakati huo, maji yamekuwa machache zaidi. Mkondo unakauka. Ardhi, ambayo tulilazimika kuiondoa maji kwa kuwa ilikuwa teketeke (swamp), imekuwa kavu sana. Tulikuwa tunachimba visima vidogo/vifupi sana kwa ajili ya kumwagilia ardhi tuliyoichukua kutoka majini. Sasa tunalazimika kuchimba chini na tunapata maji kutoka mbali zaidi. Maji ya kunywa pia yamekuwa adimu". [82]

Uzoefu wa wanajamii umekuwa ni mfano kwa wanasayansi pia. Mchoro hapo juu unaonyesha matokeo ya ufuatiliaji wa maji chini ya ardhi katika mashamba makubwa ya mikaratusi ya Mondi/ SiyaQhubeka huko Nyalazi katika pwani ya magharibi ya Ziwa St Lucia, Afrika Kusini, ambayo pia iko katika Eneo la Urithi wa Dunia. Katika kipindi cha zaidi ya miaka 13, kiasi cha maji yaliyo chini ya ardhi kwenye mashamba hayo kimeshuka kati ya 10m na 16m, ikilinganishwa na mita 4.5-7.3 tu chini ya uoto wa asili ulio karibu, ambao utakuwa umeathirika na kiwango cha chini zaidi cha maji chini ya mashamba hayo.

Nchini Kenya, kutokana na uzoefu wa matatizo ya mashamba makubwa ya mikaratusi, mwaka 2009 Waziri wa Mazingira, John Michuki, aliamuru kuondolewa kwa miti ya mikaratusi kutoka maeneo oevu na kupiga marufuku upandaji wao kando kando ya mito na mikondo ya maji. Wakati huo huo, mshindi wa nishani ya Nobeli marehemu Wangari Maathai aliomba upigaji marufuku wa upandaji wa aina ya miti ya kigeni, hasa mikaratusi, vile vile wataalam kutoka Kituo cha Kimataifa cha Utafiti wa Kilimo Misitu (ICRAF) chenye makao nchini Kenya walitahadharisha kuhusu tabia ya "kiu" ya miti ya mikaratusi[83].

Mara nyingi kinachopuuzwa katika mjadala wa maji ni kuhusu viwanda vya massa ambavyo pia hutumia kiasi kikubwa cha maji safi, na hii ndiyo sababu inayofanya viwanda hivyo kuwa juu au karibu na mito au maziwa. Maji yaliyochafuliwa kutokana na usindikaji wa mbao kwa ajili ya kutengeneza karatasi (maji machafu yanayotoka kiwandani) ambayo kisha hutiririshwa kwenye mito, maziwa au bahari, yakiwa na matokeo dhahiri hasi kwa viumbe wote wa majini na baharini ikiwa ni pamoja na samaki. Hii kwa upande mmoja hudhoofisha wanajamii ambao wanategemea vyanzo hivi vya maji kwa ajili ya matumizi pamoja na uvuvi na uvunaji wa rasilimali za baharini kama sehemu ya maisha yao. Kwa mfano, kiwanda cha massa cha Portucel kimepangwa kujengwa katika Mocuba katika jimbo la Zambezia nchini Msumbiji, ambapo mto Licungo unatumika sana na wanajamii kwa madhumuni mbalimbali.

Mto Licungo ni chanzo muhimu cha riziki kwa watu wanaoishi kando ya kingo zake. Maji yake yanatumika kwa ajili ya kupikia, kuoga, mahitaji ya mifugo, nk na kuvua samaki bila shaka.

82 http://wrm.org.uy/books-and-briefings/a-study-of-the-social-and-economic-impacts-of-industrial-tree-plantations-in-the-kwazulu-natal-province-of-south-africa

83 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section2/mounting-pressure-against-eucalyptus-in-kenya-described-as-the-water-guzzler/

Ushirikiano wa kibiashara – chanzo cha nje cha uzalishaji magogo

Kutoa 'ushirikiano' kwa wanajamii ni mbinu inayozidi kutumiwa na makampuni ili kukabiliana na malalamiko ya jamii kwamba hawapokei faida kutoka kwenye mashamba makubwa ya miti ambayo yamevamia ardhi waliyotumia kupanda mazao. Hata ajira zinazotolewa na kampuni mara nyingi ni za muda mfupi na hawalipwi vizuri, kama ilivyoelezwa hapo juu.

Mradi wa Green Resources katika jimbo la Nampula, Msumbiji, (Lurio Green Resources) umefanya 'ubia' katika miradi endelevu ya mbao na mkaa, kwa wanakijiji ambao wanatakiwa lazima wapande miti ya mikaratusi katika ardhi zao. Mradi huu unaungwa mkono na Umoja wa Ulaya. (Angalia chini)

Bango hili la Green Resources linasema: "Mradi wa uzalishaji endelevu wa kuni na mkaa. Unaofadhiliwa kwa ushirikiano kati ya Umoja wa Ulaya na Lurio Green Resources"

Kundi la washiriki katika mpango huu lilieleza kuwa walijiunga kwasababu ya ahadi zilizowekwa na kampuni: Ilisema kuwa wangeweza kuwa matajiri na kwamba wangeweza kuendelea kupanda mazao ya chakula kati ya safu za miti ya mikaratusi. Walihakikishiwa kwamba kama 80% ya miche ya mikaratusi waliyopanda itanusurika, watapewa paneli za nishati ya jua (solar panel) ili waweze kupata huduma ya umeme. Hata hivyo, watu sasa wamechanganyikiwa. Ingawa miti mingi ilinusurika na watu wengi walipokea paneli za nishati ya jua, baadhi ya paneli hazifanyi kazi tena. Ama kwa wao kuruhusiwa kukuza mazao ya chakula kati ya miti ya mikaratusi, mwanakijiji mmoja mwanamke alielezea kuwa baada ya kupanda mihogo haikuendelea vizuri, wakati mikaratusi ilizidi kukua na kukua. Yeye aliona kwamba miti ya mikaratusi ilikuwa imesababisha udongo kukauka, na hivyo kuathiri ukuaji wa mihogo. Sasa anashangaa jinsi gani angeweza kulima chakula cha kutosha kwa watoto wake [84].

Athari za mashamba makubwa ya miti kwa wanawake

Athari kali za mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda-ITPs ambazo tayari ziko kwa jamii katika Afrika zinaathiri zaidi wanawake. Hii ni kutokana na ukweli kwamba ni wanawake katika kaya za familia za vijijini za Afrika ambao hufanya kazi kama vile kuchota maji na kuzalisha chakula, kama ulivyotolewa ushuhuda na wanawake waliotajwa hapo awali katika sura hii. Kwa mujibu wa takwimu za utafiti, katika nchi nyingi za Afrika wanawake hutoa 70% ya nguvu kazi shambani, husambaza 90% ya maji ya majumbani, na wana wajibu wa kuzalisha 60-80% ya chakula kinachotumiwa na/au kuuzwa na familia. Wanachangia kwa 100% ya usindikaji wa chakula, 80% ya uhifadhi wa chakula na usafiri, na 90% ya nguvu kazi kwa ajili ya kuandaa udongo kabla ya kupanda[85].

84 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section1/the-farce-of-smart-forestry-the-cases-of-green-resources-in-mozambique-and-suzano-in-brazil

85 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section1/new-crossroads-same-actors-the-green-economy-of-the-powerful-voices-of-resistance-of-women

Licha ya takwimu kama hizi ambazo zinaonyesha umuhimu wa wanawake kuwa na uwezo wa kuendeleza familia zao kwa kilimo, haki zao za kumiliki ardhi zina usalama mdogo zaidi kuliko zile za wanaume. Kwa mfano, nchini Tanzania, 1% tu ya wanawake wana hati miliki za ardhi za kisheria, na kama wanawake wana kazi katika mashamba ya mti, wao hubeba 'mzigo maradufu', wakati wanaingiza kipato cha chini zaidi. Hii ni pamoja na kuwa wanawajibika kwa ajili ya kutafuta chakula na maji, na kuwatunza watoto wao, wakati wanatumia muda mwingi wa siku katika mashamba makubwa. [86]

'Mipango ya uthibitishaji wa 'Misitu'

Changamoto nyingine kwa jamii zilizoathiriwa na mashamba makubwa ya miti ni kwamba licha ya athari hasi zote ambazo makampuni ya mbao husababisha, bado yanaweza kupata vyeti vya uthibitisho kuwa mashamba yao ni 'endelevu', kwa maneno mengine, yasiyosababisha au kutopelekea madhara ya kiikolojia, na yasiyokiuka haki za jamii.

Wakati jamii zinaposhiriki katika mchakato wa "uthibitishaji wa misitu", kwa kawaida wanaona wanapohojiwa na wakaguzi, au labda katika mikutano ya hadhara, kwamba licha ya ukosoaji wao wa athari hasi za mazingira na kijamii zinazosababishwa na ITPs, matatizo yao na ushahidi wa athari za mashamba makubwa wanaoutoa hauwi kikwazo kwa uthibitishaji. Sababu kuu ya ukosefu wa usawa baina ya jamii kwa upande mmoja, na makampuni na bodi zao za uthibitishaji kwa upande mwingine, ni uwezo wa wadau fulani katika kushawishi mchakato zaidi kuliko wengine na hivyo kuamua matokeo. Hata hivyo, FSC inaona kuwa 'wadau' wote wako sawa katika mchakato, ambao, kwa mfano, inapingana na ukweli kwamba Green Resources ina mashamba yake ya miti katika Msumbiji yaliyothibitishwa na FSC licha ya athari zake za wazi, kama ilivyothibitishwa na malalamiko ya wanakijiji mbalimbali kwa mwakilishi wa WRM wakati wa ziara ya mashambani mwaka 2015.[87] Hali kama hiyo ilipatikana kwa watafiti wa Timberwatch walipotembelea miradi ya mashamba makubwa ya Green Resources kusini mwa Tanzania mwaka 2010.

Mfano dhahiri wa kwanini inaonekana hakuna kitu kinachoweza kufanyika ili kuzuia kampuni ya mashamba makubwa ya miti kupata uthibitisho wa FSC, ni kama ule uliotajwa kabla wa kampuni ya Uingereza iitwayo New Forests Company nchini Uganda. Mwaka 2011, ripoti ya OXFAM ilishutumu kwamba kati ya mwaka 2006 na 2010, watu 22,000 walikuwa wamefukuzwa kutoka katika ardhi yao katika wilaya za Kiboga na Mubende kama matokeo ya mradi wa shamba kubwa la Misitu Mipya, ambao ulikuwa umethibitishwa na FSC. Katika kujibu shutuma za kufukuzwa watu hao, FSC iliweka wazi mwaka 2010 kwamba: "kampuni imefuata njia za amani na ilitenda kwa kuwajibika".[88]

Kutengwa kwa jamii

Moja ya changamoto kubwa kwa jamii barani Afrika ambazo wanalazimika kukabiliana na mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda katika ardhi zao ni kuepuka kutenganishwa na kupata msaada kwa ajili ya kuimarisha harakati zao za upinzani. Mashirika ya kiraia na harakati za kijamii ni nadra kuwa hai katika maeneo ya vijijini ambako makampuni ya mashamba makubwa huvamia ardhi ya jamii. Wakati huo huo, ambacho kinaweza kusaidia sana ni kwa jamii zilizoathiriwa kutafuta njia za kufanya harakati zao zionekane na kuungana na jamii nyingine ambazo zina uzoefu wa hali hiyo.

Kwa mfano, ziara ya mwaka 2009 ya ujumbe kutoka Brazil katika wilaya kadhaa kaskazini mwa Msumbiji ambapo jamii zilianza kupata uzoefu wa uvamizi na mashamba makubwa ya miti, ilileta mabadiliko makubwa kwa jamii hizi. Kiongozi wa jamii ya watu weusi wa Brazil mwenye uzoefu wa miaka 30 juu ya athari za mashamba makubwa ya miti, na ushiriki wake kikamilifu katika harakati za kurejesha ardhi zao, alishirikisha uzoefu wake kwa zaidi ya jamii 10 katika kipindi cha wiki mbili.

86 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section1/new-crossroads-same-actors-the-green-economy-of-the-powerful-voices-of-resistance-of-women

87 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section1/the-farce-of-smart-forestry-the-cases-of-green-resources-in-mozambique-and-suzano-in-brazil/

88 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section2/uganda-new-forests-company-fsc-legitimizes-the-eviction-of-thousands-of-people-from-their-land-and-the-sale-of-carbon-credits/

Hii ilifuatiwa na viongozi wawili wa wakulima wadogo kutoka Msumbiji kutembelea Brazil kujifunza kuhusu athari za miongo kadhaa za mashamba makubwa ya mikaratusi kwa wakulima wadogo wa ndani katika Brazil, na pia juu ya harakati zinazoendelea za jamii ili kurejesha udhibiti wa ardhi yao na kuanza tena kuhuisha 'maisha' kwenye ardhi yao, ambayo inamaanisha chakula, na siyo mikaratusi. Pia walishirikishana uzoefu wao wa kuwaandaa wakulima na ujumbe wa Msumbiji, kwa upande wake, ulishirikishana uzoefu wa harakati za wakulima wadogo wadogo wa Msumbiji.[89]

Wanajamii katika maeneo ya mbali ya vijijini Msumbiji, kama walivyo wakazi hawa wa kijiji katika jimbo la Niassa, walikuwa na furaha ya kupokea wanachama wa mashirika yasiyo ya kiserikali kutoka Afrika Kusini kama wageni.

Mashamba makubwa mapya ya miti huhamisha mifugo ya jamii kutoka katika maeneo yao ya zamani ya malisho, na pia kusababisha 'ukame wa ndani' ambao unapunguza upatikanaji wa maji na mimea inayoliwa.

[89] The visits were facilitated in 2009 and 2010 by the international secretariat of the WRM, in collaboration with UNAC in Mozambique and the Via Campesina and traditional communities in Brazil.

6. Hitimisho

Kuhusu suala la mashamba makubwa ya miti katika Afrika, makampuni washirika wa ushauri katika sekta hii, benki za maendeleo na watafiti huwa wanadai kwamba nchi za Kiafrika zinahitaji sana vyanzo mbadala vya mbao - hasa mbao zilizochanwa katika maumbo na saizi tofauti na kuni au mkaa - kwasababu wakazi wengi wanaongezeka haraka na makazi yao yanazidi kuwa ya mjini. Wanasema kuwa nchi nyingi za Afrika zinaweza hata kuwa na haja ya kuagiza mbao katika siku zijazo.

Ufumbuzi wanaouwakilisha ni kwamba kama nchi zinataka kuokoa misitu yao kutokana na uvunaji, basi zinapaswa kukuza mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda. Kwa wale wenye wasiwasi kuhusu athari hasi zinazosababishwa na mashamba makubwa ya miti, majibu ya kawaida ni kwamba ni tatizo la 'usimamizi' na wao wanasema kuwa kama serikali zingeliwezesha ushirikishwaji wa sekta binafsi zaidi, mashamba makubwa yangeweza kupangwa na kusimamiwa vizuri zaidi, na hivyo kupunguza hatua kwa hatua athari hizi. Kwa kiasi fulani umekuwa ni ujumbe huo huo katika propaganda zinazotumiwa na makampuni makubwa yanayohamasisha mashamba makubwa ya miti katika Afrika. Hata hivyo, ukweli unaonyesha kwamba si tatizo la 'usimamizi' - athari zinazoweza kutokea kwa jamii na mazingira ya asili zinaendelea bila kujali uzuri wa mameneja wanaoweza kuudai, au hata kama mashamba makubwa yatakuwa yamethibitishwa na FSC!

Haiwezi ikakanushwa kuwa kuna mahitaji yaliyopo na yanayongezeka ya kuni na mbao barani Afrika. Hata hivyo, upandaji wa kiwango kidogo cha miti inayofaa ya asili itafaidisha jamii kwa kutoa vitu vingi muhimu na huduma, kwa mfano, mbao kwa ajili ya ujenzi wa makazi na kutunza vyanzo vya maji. Hata hivyo, taarifa hii inaibua maswali muhimu kuhusu mapendekezo kutoka Benki ya Dunia, makampuni ya ushauri wa kitaalamu na watafiti wa sekta yenyewe juu ya nini kifanyike: Kupanua mashamba ya miti, yanayomilikiwa na makampuni, yanayoendeshwa kwa faida, kiwango kikubwa cha kilimo cha miti ya aina moja, ambacho kwa kawaida ni chenye madhara ya kiikolojia na aina ngeni vamizi ya miti kama mikaratusi.

Uzoefu wa miradi ambayo maamuzi hufanyika kabla ya kushirikisha ngazi ya chini na inayoendeshwa kwa faida ya "upandaji upya wa miti" na "upandaji tena wa miti" katika mataifa ya kusini - na AFR100 inaonekana kuwa na sifa nyingi zinazofanana - inaonyesha kwamba, mwisho wa siku, miradi kama hiyo hunufaisha hasa makampuni ya kigeni, mifuko ya uwekezaji na washauri wataalam, wakati wengi wa jamii hasa za vijijini zinazoishi ndani na kuzunguka maeneo yaliyoathirika na upanuzi wa mashamba ya miti huwa zinaachwa bila ardhi ya kutosha, chakula na maji. Wanaponyimwa mahitaji ya msingi yanayohitajika kwa ajili ya kuendesha maisha yao, watu maskini wa vijijini mara nyingi hulazimika kuhamia katika makazi duni yasiyokuwa rasmi 'yasiyopimwa' karibu na miji midogo au miji mikubwa.

Mwenendo wa sasa wa kupanua mashamba makubwa ya miti katika mashariki na kusini mwa Afrika unaonyesha, kwa mara nyingine tena, haja ya haraka ya kuwa na mchakato tofauti ambao ni rafiki kwa watu kwa ajili ya "urejeshaji wa ardhi katika hali yake ya awali", si unaoendeshwa kwa ajili ya faida ya kampuni au rushwa, lakini unaoongozwa na jamii na kutekelezwa kwa namna ambayo wao wanaamini inahitajika ili kuboresha maisha na ustawi wao, wakati huo huo ikilinda mazingira na kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali. Aidha, ardhi ya jamii ambayo imevamiwa na mashamba ya miti irudishwe kwa wanajamii. Kuna mifano kutoka Brazil, Thailand na Indonesia, ambapo mashamba makubwa ya miti yamebadilishwa tena kuwa ardhi inayotumika kama ilivyofafanuliwa kulingana na maslahi na vipaumbele, na inadhibitiwa na jamii.

Mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda tayari yameshachukua kiasi kikubwa cha ardhi nzuri katika mashariki na kusini mwa Afrika, ikiwa na athari mbaya kwa rasilimali za maji, udongo na bioanuai. Kama mashamba makubwa hayo kwa ajili ya viwanda yatapanuka zaidi, ndivyo hivyo athari zake za uharibifu zitakavyoenea zaidi katika mazingira na jamii, na kulazimisha wanyamapori na watu kuingia kwenye ardhi za pembezoni zenye uzalishaji mdogo katika maeneo kame. Mbali na kuwa ni shughuli ya 'kijani', mashamba makubwa ya miti kiuhalisia, ni kama kuchimba madini, shughuli za utoaji wa malighafi kutoka ardhini.

Yote hufanyika kwa jina la "maendeleo ya jamii" na/au kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, wakati katika hali halisi ina athari kinyume na hayo yanayokusudiwa; huendesha uzalishaji kwa ajili ya viwanda unaoongezeka na matumizi ya ziada kimataifa. Hii inaweza tu kuzuru zaidi kile kilichoachwa kwenye mazingira ya asili. Kuna njia zenye uharibifu mdogo za kuishi, kama zilivyoonyeshwa wazi na jamii katika mataifa ya Kusini mwa dunia ambazo zimekuwa zikiishi kwa njia endelevu, na kwa amani na mazingira asili, kwa maelfu ya miaka.

Ulimwengu mwingine unawezekana!

World Rainforest Movement na Timberwatch Coalition

Kiambatanisho: Nchi zilizoko kwenye mapitio

a) Afrika Kusini, Swaziland na Lesotho (Kusini)

1) Afrika Kusini

Kuna hali ya kutokuwa na uhakika kuhusu eneo halisi la mashamba makubwa ya miti nchini Afrika Kusini. Kwa mujibu wa vyanzo vya sekta hiyo kuna hekta zipatazo milioni 1.27[90] chini ya mashamba makubwa ya mbao kwa ajili ya viwanda. Hata hivyo, eneo liliotajwa katika ripoti ya FAO ya FRA2015 ni kubwa zaidi, kufikia hekta milioni 1.76 za " misitu ya kupandwa " (angalia jedwali katika ukurasa wa 9). Kuna eneo sawa na hilo (wastani wa hekta milioni 1.7) zaidi zikiwa za nyanda za nyasi za asili na ardhi oevu ambayo imeathirika na aina ngeni za migunga (miwati), mikaratusi na misindano, ambayo imeruhusiwa kuenea kutoka katika mashamba makubwa ya miti ambayo yamesimamiwa vibaya au yaliyotelekezwa.[91]

Hivi sasa serikali ya Afrika Kusini in lengo la kuwa na hekta 10,000 za mashamba makubwa mapya ya miti yatakayoanzishwa kwa mwaka, kwa takriban miaka kumi. Maeneo makuu yaliyolengwa ni kusini mwa KwaZulu-Natal na sehemu ya kaskazini ya jimbo la Rasi ya Mashariki, yenye lengo la kusambaza magogo zaidi ya mikaratusi kwa sehemu ya kiwanda kinachomilikiwa na serikali cha Sappi SAICCOR cellulose kwa ajili ya mahitaji ya baadaye ya malighafi. Kwa miaka kadhaa pia kumekuwa na majadiliano ya kuwa na kiwanda kipya cha massa huko Mthatha katika Rasi ya Mashariki.

Washugulikaji wakuu katika sekta hii ni:
SAPPI Kusini mwa Afrika: [92] Kampuni kubwa ya kimataifa yenye viwanda 4 vya massa nchini Afrika Kusini, pamoja shughuli za uzalishaji wa massa na karatasi katika Marekani na Umoja wa Ulaya. Mashamba yake husambazia viwanda vyake vikubwa viwili vya (SAICCOR & Ngodwana) na viwili vidogo vya (Stanger & Thukela) ambavyo hasa huzalisha massa ya celulosi (cellulose pulp) kwa ajili ya kuuza nje. Hii ni sawa na kusafirisha nje maji, bioanuai, hewa safi ya Afrika Kusini na udongo. Sappi[93] ina mashamba makubwa ya mbao yenye eneo la hekta 492,000.

Mondi PLC: Hii ni kampuni nyingine ya kimataifa, yenye zaidi ya hekta 307 000 za mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda, yaliyolundikana katika jimbo la KwaZulu-Natal, ambapo ina viwanda vikubwa viwili vya massa na karatasi, katika Ghuba ya Richards na Durban. Mondi pia ina mashamba makubwa ya miti katika Urusi. Mondi imejaribu 'kutia kasumba ya kijani' shughuli zake kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) ya uhifadhi, WWF na WESSA kupitia "Programu ya maeneo oevu ya Mondi (Mondi Wetlands Programme)", na "mradi wa kizazi kipya cha mashamba makubwa ya miti (New Generation Plantations)" wa WWF.

SAFCOL/Komatiland: Hii kampuni inayomilikiwa na serikali ambayo inalenga katika kupanda miti ya misindano kwa ajili ya usindikaji wa magogo na shughuli zinazohusiana na hizo. Mwaka 2013, kampuni hii ilikuwa na hekta 187,320 za mashamba ya miti katika ardhi inayomilikiwa na serikali. SAFCOL pia inamiliki 80% ya IFLOMA[94] katika jimbo la Manica nchini Msumbiji.

Makampuni yote mawili ya Sappi na Mondi yana 'miradi ya wakulima wa nje wa mkataba' ambayo inawaruhusu wao kupata ardhi ya jamii, bila kulipa kodi na kuwajibika kifedha ikiwa mashamba makubwa yatashindwa. Uungaji mkono kifedha wa serikali ya Afrika Kusini katika SAPPI na SAFCOL unagongana na majukumu yake ya kusimamia sekta vizuri katika utekelezaji wa sheria zinazosimamia matumizi ya maji na athari za mazingira. Kiutendaji jukumu hili linafanywa chanjo cha nje yaani FSC, lakini kwasababu bodi nyingi za uthibitishaji na wakaguzi wao wana maingiliano na maafisa wa serikali au sekta hiyo, na kwa kuwa wanalipwa moja kwa moja na makampuni yanayokaguliwa, haiwezekani kwa wao kutokuwa na upande wowote kikamilifu, na kufanya ukaguzi bila upendeleo. Angalia ripoti husika katika www.facebook.com/GeaSphere.

---

90 http://www.gov.za/about-sa/forestry
91 http://www.timberwatch.org.za/index.php?id=99
92 www.banktrack.org/manage/ems_files/download/sappi_profile_by_timberwatch_0_pdf/sappi_profile_by_timberwatch_0.pdf
93 http://www.sappi.com/regions/sa/SappiSouthernAfrica/Sappi%20Forests/Pages/default.aspx
94 http://www.panapress.com/South-African-outfit-takes-over-Mozambican-timber-company--13-544306-17-lang2-index.html

Shughuli nyingine za uendeshaji wa mashamba makubwa ya miti Afrika Kusini

NCT Forestry Co-operative Limited ni kampuni ya usimamizi ambayo inauza mbao kutoka kwa wakulima binafsi na mashamba yake yenyewe kutoka katika jumla ya hekta 300,000 – ambazo ni 21% ya mashamba makubwa ya miti nchini Afrika Kusini.

Cape Pine Investment Holdings (MTO) [95] inayomilikiwa na Mfuko wa Mazingira Duniani, ina hekta 53,000 za mashamba ya misindano katika ya ardhi inayomilikiwa na serikali katika Jimbo la Rasi ya Magharibi.

Global Forest Products - pia inayomilikiwa na Mfuko wa Mazingira wa Duniani, yenye jumla ya eneo la hekta 90,000 za mashamba ya miti katika jimbo la Mpumalanga.

Ramanas Farms katika eneo Sabie, Jimbo la Mpumalanga - pia yanayomilikiwa na Mfuko wa Mazingira wa Kimataifa, ina jumla ya hekta 8,300 za mashamba ya miti.

Imvelo Forests - pia inayomilikiwa na Mfuko wa Mazingira Duniani, ina jumla ya hekta 3671 za mashamba ya miti.

Mfuko wa Mazingira Duniani wenye makao yake nchini Marekani [96] [97] umepata shughuli ndogo ndogo kadhaa za za mashamba makubwa ya miti nchini Afrika Kusini, wakidai kuwa wanaboresha utendaji wa mazingira na faida. Wao kuwa wamethibitishwa na FSC wanachukuliwa kama ushahidi wa 'kuwajibika katika usimamizi.'

York Timber Holdings[98] iko katika jimbo la Mpumalanga, na ina hekta 60,000 za mashamba makubwa hasa ya misindano, na inatengeneza vitu vya nyumbani vitokanavyo na misindano.

Evowood (MASONITE Afrika Limited[99]): Ilikuwa inamilikiwa kwa 80% na Masonite International hadi hivi karibuni ilipouzwa kwa wawekezaji wa ndani wa Afrika Kusini. Mnamo 2015 ilikuwa na hekta 25,000 za miti katika Mkoa wa KwaZulu-Natal.

Merensky[100] yenye jumla ya eneo la hekta 69,000 za mashamba makubwa ya misindano na mikaratusi pamoja katika Rasi ya Mashariki, Majimbo ya KwaZulu-Natal na Limpopo. Maeneo haya yanajumuisha mashamba makubwa ya miti kwenye ardhi iliyokodishwa ya serikali, ambayo zamani ilikuwa inasimamiwa na serikali.

2) Lesotho

Lesotho ni nchi ndogo yenye milima ambayo imezungukwa kabisa na Afrika Kusini. Kwa mujibu wa FAO ilikuwa na karibia hekta 17,000 za mashamba ya miti ya mikaratusi na misindano[101] mwaka 2015, mengi kati ya hayo yanayomilikiwa na serikali. Baadhi ya mashamba hayo awali yalianzishwa kati ya mwaka 1973 na 1987 kama sehemu ya mradi wa shamba la timbao la Lesotho ili kutoa kuni na mbao za ujenzi. Hata hivyo, tangu mwaka 2004 uanzishwaji wa mashamba makubwa ya miti umekuwa ukihamasiswa kikamilifu nchini Lesotho na FAO chini ya kitengo chake cha NFP (Mpango wa Taifa wa Misitu) [102], lakini bila ya mafanikio.

Kusoma zaidi:

Kijarida cha NFP Facility – 2011
http://www.fao.org/forestry/25416-0bc703d8a50aa510032e1fe9609f262c0.pdf

Utafiti wa FOSA wa nchi ya Lesotho - ftp://ftp.fao.org/docrep/fao/004/AB589E/AB589E00.pdf

---

95 www.capepine.co.za

96 www.capepine.co.za

97 http://globalenvironmentfund.com/wp-content/uploads/2009/09/GEF-Whitepaper-Timberland-Investment-Emerging-Markets-A-Fresh-Review-Outlook-September-2009.pdf

98 www.york.co.za

99 http://saforestryonline.co.za/news/masonite-plantations-and-mill-up-for-sale

100 http://www.merensky.co.za

101 GLOBAL FOREST RESOURCES ASSESSMENT 2015, UN FAO, Rome, 2015 - http://www.fao.org/3/a-i4808e.pdf

101 http://www.fao.org/docrep/013/al550E/al550E.pdf

102 http://foris.fao.org/nfp-facility/public/partnership/100664.do

3) Swaziland

Hii nchi ndogo iliyopo kati ya Afrika Kusini na Msumbiji ina inakadiriwa kuwa na eneo la hekta 170,000 za mashamba makubwa hasa misindano na mikaratusi. Kama ilivyo katika Afrika Kusini, pia kuna maeneo ambayo yamevamiwa na mashamba makubwa ya miti 'yaliyotoroka' - yaani miti ambayo awali ilikuwa imepandwa mashambani na mbegu zake zikatawanyika na kukulia porini, ambayo yamemaliza kabisa rasilimali za maji na kuharibu bioanuai tajiri ya nyanda za nyasi.

Montigny Investments[103]: Ni kampuni yenye makao yake Swaziland ambayo ilinunua shughuli za Sappi ya Swaziland mwaka 2014,[104], kwa ZAR bilioni 1, ikijumuisha karibu nusu ya mashamba ya miti katika magharibi ya kati ya Swaziland (hekta 55,000) ambayo inalimwa katika ardhi ya taifa ya Swaziland iliyokodishwa kutoka serikalini, pamoja na kiwanda cha massa cha Usutu ambacho hakijafanya kazi tangu mwaka 2010.

Transvaal Wattle Growers Co-operative (TWK)[105], Kampuni ya Afrika Kusini, inayomiliki kampuni ya misitu ijulikanayo kama Shiselweni Forestry Company Ltd katika kusini mwa Swaziland, ikiwa na jumla ya hekta 12,000 za mashamba makubwa ya miti.

Peak Timbers[106], Kampuni ambayo awali ilikuwa inamilikiwa na Mondi sasa ni mali ya Mfuko wa Mazingira Duniani, na ina hekta 31,500 za vibanzi vya timbao na mashamba makubwa ya mbao na biashara ya kuchana mbao, vyote vikiwa katika mji wa Piggs Peak ulioko kaskazini magharibi ya Swaziland.

Swaziland Plantations Limited – Mashamba haya yako kusini mwa mji wa Piggs Peak, yanasambaza mbao zilizochanwa katika saizi na maumbo mbalimbali katika sekta ya ujenzi ya Afrika Kusini.

Kusoma zaidi

- Swaziland: Hadithi za mashamba makubwa endelevu ya mbao
http://wrm.org.uy/books-and-briefings/swaziland-the-myth-of-sustainable-timber-plantations

- Swaziland: Athari za miaka 50 ya misitu ya kwa ajili ya viwanda
https://chrislang.org/2005/01/24/swaziland-the-impact-of-50-years-of-industrial-forestry

Swaziland: Moto wa mashamba yaliyothibitishwa watoa cheche za dharura kwa taifa
http://www.fsc-watch.org/archives/2007/08/28/Swaziland__fires_in_certified_plantations_spark_national_emergency_

Mashamba makubwa ya mbao Swaziland
http://wrm.org.uy/oldsite/countries/Swaziland/Plantations.pdf

- Swaziland yaishutumu Sappi kwa kuiba mbao baada ya kufunga kiwanda
www.iol.co.za/business/news/swaziland-accuses-sappi-of-stealing-timber-after-closing-mill- 1138624

- Mpango wa ajira 3000 za SAPPI wafungwa
www.times.co.sz/news/98037-3-000-sappi-jobs-deal-sealed.html

---

103 http://www.montigny.co.sz
104 http://www.ujuh.co.za/exit-of-sappi-from-swaziland-usuthu-speak-volumes
105 http://www.twkagri.com
106 http://www.globalenvironmentfund.com/peak-timbers

b) Malawi, Msumbiji, Zambia na Zimbabwe (kati)

4) Malawi

Kama ilivyo kwa miradi mingine ya ukoloni katika ukanda huu, tangu mwaka 1930 Malawi ilitumika kama 'mnyama wa maabara' kwa majaribio na mashamba makubwa ya miti itoayo mafuta ya Tung nut iliyopandwa katika miinuko ya Viphya, ili kusambaza mafuta ya tung katika masoko ya Ulaya. Hata hivyo, kutokana na mahitaji yasiyojitosheleza badala yake miti ya misindano ilipandwa.

Raiply Malawi Ltd: Miti ya misindano kwenye shamba kubwa linalomilikiwa na serikali lenye hekta 53,501 katika miinuko ya Viphya, kama sehemu ya Viphya Plywood and Allied Industries (VIPLY) ilipandwa kwanza kabla ya mwaka 1964, wakati Malawi ilipopata uhuru kutoka Uingereza. Awali ilifadhiliwa na shirika la Ukoloni la Maendeleo (baadaye Jumuiya ya Madola) (CDC), sehemu ya shamba la VIPLY baadaye ilichukuliwa na Raiply[107] kutoka Kenya, pamoja na upatikanaji wa kipekee wa hekta 20,000 kupitia mkataba wa umiliki wa miaka 15 wa mwaka 1998. Hekta 33,000 zilizobaki za misindano ziliwekwa akiba kwa ajili ya wavunaji magogo wenye leseni wa Malawi, lakini sasa inaonekana kwamba eneo hili limevunwa likaisha bila upandaji tena wa kutosha unaofanyika, na wavunaji magogo sasa wameshaanza kuingilia kwenye eneo la milki ya Raiply.

Citrefine Plantations Ltd[108] inayofanya biashara kama Kawandama Hills Plantation[109] - Hii ni kampuni inayozalisha mafuta muhimu (essential oil) ambayo ina mpango wa kupanda mikaratusi na miti mingine migeni katika hekta 5,700 za ardhi mpya iliyobakia ya nyanda za nyasi yenye vichaka vya miti ya asili katika sehemu ya miinuko ya Viphya. Mradi huo umefadhiliwa kwa Msaada wa Marekani unaofikia dola za Marekani 309,000 [110]

Uharibifu wa muda mrefu ya kiikolojia, ukame na moto mkali wa mwituni unaosababishwa na mashamba ya miti katika miinuko ya Viphya ni mfano ya miradi ya shirika la Ukoloni la Maendeleo (baadaye Jumuiya ya Madola) CDC katika kanda hii kama vile Bhunya katika Swaziland. Hii ni kutokana na kucheza 'kamari' na majaribio kwa kutumia maliasili na fedha za watu wengine.

Kusoma zaidi

http://www.theafricareport.com/Southern-Africa/logging-and-deforestation-malawis-diminishing-plantations.html

http://www.times.mw/k2-billion-lost-in-viphya-plantations/

http://www.nyasatimes.com/loggers-encroaches-raiply-timber-concession-area/

http://www.sde.co.ke/thenairobian/article/2000201533/the-immortals-from-timber-the-rai-family-became-billionaires

https://afrosai-e.org.za/sites/afrosai-e.org.za/files/report-files/Viphya%20Performance%20Audit%20report%20tabled%20in%20Parliament%202%2D ec%202011.pdf

- FAO FRA 2010 – Malawi http://www.fao.org/docrep/013/al557E/al557E.pdf

107 http://www.sde.co.ke/thenairobian/article/2000201533/the-immortals-from-timber-the-rai-family-became-billionaires

108 https://www.growafrica.com/organizations/citrefine-plantations-limited

109 http://www.kawandama-hills.com

110 http://newswatchreviews.com/citrefine-plantations-limited-malawi-in-action

5) Msumbiji

Msumbiji ina kiwango cha juu cha upanuzi wa ITP katika kanda hii. Kwa mujibu wa FAO[111], mwaka 2010 ilikuwa na jumla ya hekta 62,000 za mashamba makubwa ya miti, lakini ilipofika mwaka 2015 zilikuwa zimeongezeka hadi kufikia hekta 75,000, hasa mikaratusi na misindano. Inakadiriwa kuwa zaidi ya hekta nusu milioni ziko chini ya udhibiti wa makampuni ya mashamba makubwa ya miti yakiwa na makubaliano na serikali ya kupanda maeneo makubwa zaidi katika miaka ijayo. Hata hivyo, kuna vikwazo ambavyo vinaweza kuzuia hili lisitokee, ikiwa ni pamoja na ongezeko la upinzani kutoka kwa jamii zilizoathiriwa, na kupungua kwa mahitaji kutoka katika mataifa ya Kaskazini, kutokana na hali mbaya ya kifedha katika nchi zenye viwanda vingi.

Makampuni makuu ya mashamba makubwa ya miti

Green Resources (GR): Ni kampuni ya Norway ambayo tangu mwaka 2005 - 2009, ilipewa milki ya matumizi ya ardhi kwa karibu hekta 264,898 katika majimbo matatu ya Nampula, Niassa na Zambezia. Mwaka 2014 GR iliungana na GSSF kuunda kampuni kubwa kuliko zote ya mashamba makubwa nchini, lakini imeripotiwa kwamba GR ina matatizo ya kifedha.

Portucel ni kampuni ya Kireno ya massa na karatasi ambayo ina mipango ya kuanzisha kiwanda kikubwa cha massa kwa msaada wa Benki ya Dunia/IFC. Mradi mzima unahusisha upandaji wa hadi hekta 356,000 za ITPs katika majimbo ya kati ya Zambezia na Manica. Hivi sasa sehemu ndogo tu ya hii imepandwa.

Florestas de Niassa katika kaskazini-magharibi mwa Msumbiji inamilikiwa na shirika la Bonde la Ufa la Afrika (African Rift Valley Corporation). Ina hekta 7,000 za misindano na mikaratusi lakini ina mipango ya kupanda hekta 60,000.

IFLOMA (Industrias Florestais de Manica) ina hekta 19,000 za mashamba makubwa ya miti katika Jimbo la Manica karibu na mpaka wa Zimbabwe. 80% ya IFLOMA ni mali ya serikali ya Afrika Kusini (Komatiland), na nyingine ni ya serikali ya Msumbiji.

Kusoma zaidi

- Mabwana wa ardhi – Uchambuzi wa mwanzo kuhusu tukio la uporaji wa ardhi http://www.unac.org.mz/yootheme/widgetkit/LordOfTheLand.pdf
- Upanuzi wa kilimo cha miti ya aina moja nchini Msumbiji – Athari kwa jamii za wakulima wa kujikimu wa ndani katika Jimbo la Niassa- http://wrm.org.uy/books-and-briefings/the-expansion-of-tree-monocultures- in-mozambique-impacts-on-local-peasants-communities-in-the-province-of-niassa
- Makala iliyochapishwa katika jarida la kila mwezi la WRM kuhusu athari kwa jamii za ndani za upanuzi wa mashamba makubwa.
- http://wrm.org.uy/browse-by-country/africa/mozambique/#Articles%20from%20the%20WRM%20Bulletin
- Green Resources ilipoteza karibia dola za Marekani milioni 70 katika kipindi cha miaka miwili kwenye miradi yake ya Msumbiji http://zitamar.com/norwegian-forestry-firms-losses-mount-mozambique-acquisitions
- "o Avanço das Plantações Florestais sobre os Territórios dos Camponeses no Corredor de Nacala: o caso da Green Resources Moçambique"

  https://issuu.com/justicaambiental/docs/o_caso_da_green_resources_moc__ambi

111 http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section1/mozambique-industrial-tree-plantations-generate-profits-for-investors-negative-impacts-for-peasant-communities

6) Zambia

Zambia ina karibu ya hekta 64,000 za mashamba makubwa ya miti ambazo hekta 55,000 zilianzishwa katika mkoa wa Copper Belt katika miaka ya 1960 kwa msaada wa Benki ya Dunia na IDC.[112] Mwaka 2013 Serikali ilizindua Mpango wa Taifa wa Upandaji Miti[113] kwa lengo la kupanda hekta 20,000 hasa za mashamba makubwa ya misindano na mikaratusi.

Inaonekana kwamba kumekuwa hakuna wajibu wa kurejesha misitu au kupanda tena upya, lakini hii inaweza hivi karibuni kubadilika kama sheria za kupanda tena upya miti ya kigeni katika mashamba makubwa zitaanzishwa. Hata hivyo, hii inaweza kusababisha kupotea kwa mapori ya asili ambayo kwa kawaida hurudia katika hali yake ya asili kwa muda baada ya kuvuna magogo kwa ajili ya mbao au mkaa, na wanajamii bado wanaweza kutumia ardhi kupanda mazao, pamoja na kukusanya mimea ya madawa na vifaa vya ujenzi ambavyo visingewezekana baada ya mashamba ya miti kuwa yameanzishwa.

Ni nani anayekuza mashamba makubwa nchini?

- **Shirika la elimu ya Misitu na Viwanda vya Misitu la Zambia (ZAFFICO)[114]**: Ni kampuni inayomilikiwa na serikali ya Zambia. ZAFFICO ilimiliki hekta 55,000 za awali za mashamba makubwa hadi miaka ya 1990 wakati ilipouza hekta 2,000 kwa wamiliki binafsi.

Kusoma zaidi:

http://www.parliament.gov.zm/sites/default/files/images/publication_docs/Ministerial%2009th%20Nov%20-%20Wilbur.pdf

7) Zimbabwe

Mpaka mwaka 2015, Zimbabwe ilikuwa na hekta 87,000 za mashamba makubwa ya miti kwa mujibu wa FAO, lakini vyanzo vya ndani hutoa takwimu za juu zaidi za hekta168,000[115]. Mengi ya mashamba makubwa ni ya misindano na asilimia ndogo ya karibu 15% ni mikaratusi na miwati.

42% ni mali ya serikali kupitia Tume ya Misitu; 54% inamilikiwa na makampuni binafsi na salio ni mali ya wakulima wadogo binafsi ikiwa ni pamoja na vyama vya ushirika.[116]

Nani anayekuza mashamba makubwa ya miti nchini?

- **Borders Timbers**[117]: Kampuni hii inadhibiti eneo la hekta 28,000, na Misindano ikiwa aina kuu ya miti iliyopo. Kampuni hii ni mali ya Rift Valley Corporation, kampuni ya kiafrika yenye shughuli zake katika nchi kadhaa.

- **Allied Timbers**[118] – Ni kampuni inayomilikiwa na serikali yenye hekta 12,000 katika maeneo matatu. Ina mipango ya kurekebisha, na kisha kupanua mashamba makubwa kwa lengo la kuongeza mauzo ya nje.

---

112 http://www.worldbank.org/projects/P003155/forestry-project?lang=en

113 http://theredddesk.org/countries/initiatives/national-tree-planting-programme

114 http://www.zaffico.co.zm/index.php/2013-06-05-18-35-22

115 http://www.zimbabwesituation.com/news/zimsit_g_forestry-firms-urged-to-co-exist-with-villagers

116 http://www.fao.org/docrep/004/AC429E/AC429E04.htm

117 http://www.bordertimbers.com/forestry.php

118 http://www.thestandard.co.zw/2016/03/20/allied-timbers-workers-bear-brunt-of-firms-rot

c) Kenya, Tanzania and Uganda

8) Kenya

Kunaonekana kuwa kuna taarifa kidogo za kuaminika juu ya eneo lililo chini ya mashamba makubwa ya miti nchini Kenya, ingawa FAO (FRA2015) inatoa jumla ya hekta 220,000. Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni, eneo la mashamba makubwa ya miti ya serikali ni hekta 125,000. Mbali na hayo pia kuna mashamba makubwa ya miti yanayomilikiwa na serikali chini ya usimamizi wa Halmashauri za Wilaya, maeneo ambayo bado hayajawekewa kumbukumbu. Mashamba makubwa ya miti yanayomilikiwa binafsi huchukua eneo linalokadiriwa kufikia hekta 150,000. Hizi ni pamoja na zile zinazomilikiwa na makampuni binafsi kama vile Mashamba ya Chai, Kakuzi, na makampuni ya tumbaku (hasa British American Tobacco na Mastermind Ltd) ambayo hutumia kuni kama chanzo cha joto kwa ajili ya kukausha majani ya tumbaku.[119] Miti aina ya misindano na mikaratusi hupandwa zaidi.

Nani anayekuza mashamba makubwa ya miti?
Benki ya Dunia imekuwa msaidizi mkuu wa uanzishwaji wa mashamba makubwa ya miti nchini na kwa sasa kuna mradi mwingine wenye lengo la kusaidia Wakala wa Misitu wa Kenya (Kenya Forest Service). Pia mtendaji katika kusaidia sekta ya mashamba makubwa ya miti katika Kenya ni Serikali ya Ufini kupitia mradi wa Miti Mingi Maisha Bora (MMMB), kwa lengo la kutoa msaada katika mchakato wa mageuzi yanayoendelea ya sekta ya misitu. Washirika wengine wanaosaidia ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mfumo wa Umoja wa Mataifa, kwa mfano, kupitia Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP), na wafadhili kama vile Denmark, Marekani na Japan. Nyingi ya fedha hizo zinatolewa kusaidia shughuli za jumla, ambazo ni pamoja na mashamba makubwa ya miti.[120]

Kusoma zaidi:
- Kenya: Wakala wa Misitu kuiokoa mikaratusi
http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section3/kenya-the-forest-service-to-the- rescue-of-eucalyptus

- Shinikizo dhidi ya mikaratusi katika Kenya, iliyoelezewa kama inayofyonza maji kwa pupa
- http://wrm.org.uy/articles-from-the-wrm-bulletin/section2/mounting-pressure-against-eucalyptus-in-kenya-described-as-the-water-guzzler

- Wangari Maathai: Punde tu kabla ya kifo chake aliandika kuhusu uhusiano uliopo katika “Misitu iliyotulia” ya mashamba makubwa ya mikaratusi na njaa iliyosababishwa na ukame mkali zaidi, mabadiliko ya tabia nchi na upotevu wa bioanuai katika Kenya.
See www.theguardian.com/commentisfree/2011/nov/25/silent-forests-famine-east-africa

- Kenya kupanda ‘vazi la kijani’ lenye ukubwa/saizi ya Costa Rica

Na Katy Migiro, Reuters, 8 Septemba 2016

"Kenya ina lengo la kurejesha miti na uoto karibu asilimia tisa ya ardhi yake ifikapo mwaka 2030", serikali ilisema hayo siku ya Alhamisi, katika mpango wake kabambe wa kupambana na mabadiliko ya tabianchi, umaskini na njaa. Hekta milioni 5.1 za ardhi iliyokatwa miti ovyo na kuharibiwa iliyolengwa kwa ajili ya mazingira na urejeshaji wa misitu ni sawa na ukubwa wa Costa Rica katika Amerika ya Kati. "Mpango huu unaonyesha jitihada madhubuti na utaratibu mzuri zaidi wa kurejesha misitu iliyoharibiwa na mandhari nyingine," Waziri wa mazingira wa Kenya Judy Wakhungu alisema katika uzinduzi wa mradi."

---

119 http://www.sifi.se/wp-content/uploads/2012/02/Forest-plantations-and-woodlots-in-Kenya.pdf

120 http://www.finland.or.ke/public/default.aspx?nodeid=46392&contentlan=2&culture=en-US

9) Tanzania

Tanzania inakadiriwa kuwa na hekta 290,000 za mashamba makubwa ya mbao. Kati ya hizi karibia hekta 85,000 zinamilikiwa na serikali. Mashamba makubwa yanayomilikiwa binafsi hufunika takriban hekta 200,000.[121]

Hadi kufikia mwishoni mwa miaka ya 1990, sera ya taifa ya misitu ilipitiwa upya na matokeo ya mchakato huu ni kupitishwa kwa sheria mpya (Sheria ya Misitu nr.14 ya 2002) ili kukuza ushiriki wa sekta binafsi katika kuanzisha mashamba makubwa ya miti zaidi. Utekelezaji wa sera hii mpya uliungwa mkono na Benki ya Dunia.

Aina ya miti muhimu zaidi katika mashamba makubwa kwa ajili ya viwanda ni misindano, misonobari, mikaratusi na tiki. Mengi ya mashamba makubwa ya miti yanayomilikiwa na serikali na watu binafsi ni ya misindano, ambayo huchukua karibia 78% ya eneo lote lililolimwa. Katika kipindi cha 'kukimbilia dhahabu' ya jatropha ili kuzalisha biodiseli (nishati kimiminika itokanayo na mimea) kilipomalizika, maelfu ya hekta yalikuwa yamepandwa, lakini nyingi kati ya hizo huenda zikatelekezwa, au kubadilishwa kwa miti mingine au mazao.

Nani ambaye anakuza mashamba makubwa ya miti?

Kampuni ya Miwati ya Tanganyika (Tanganyika Wattle Company - TANWAT) katika Wilaya ya Njombe ina karibu hekta 14,500.
Green Resources Ltd (GR) inadhibiti hekta 74,000 katika Nyanda za Juu Kusini, ambazo hekta 12682 zimepandwa. GR ni kampuni ya Norway yenye miradi mingine nchini Msumbiji, Uganda, na Sudan Kusini. Mashamba yao ya miti yana malengo kwa ajili ya matumizi mbalimbali, kuanzia mbao mpaka fidia ya hewa ukaa, ingawa wamekosolewa kwa kuuza nyongeza ya hewa ukaa isiyoaminika. [122] Mwaka 2011 baadhi ya mashamba yao yalithibitishwa na FSC.
Kiwanda cha Karatasi Mufindi wilayani Mufindi. Hiki ndicho kiwanda pekee cha massa nchini, na uwezo wake kwa mwaka wa tani 60,000 za karatasi nene kama ubao mwembamba (Kraft), lakini kuna mipango ya kupanua uwezo wa uzalishaji wa tani 100,000/mwaka. Kiwanda cha Karatasi cha Mufindi kina hekta 10,000 za mashamba ya mikaratusi.
Kilombero Valley Teak Company (KVTC), ina eneo la ardhi la hekta 28,000 mkoani Morogoro kusini mwa Tanzania. Wanahisa wakuu wa KVTC ni Mfuko wa Mazingira Duniani kutoka Marekani ambao una uwekezaji wa mbao katika nchi kadhaa za Afrika, na Mfuko wa Maendeleo wa Ufini[123].
The New Forest Company (NFC) ni kampuni yenye makao yake London na shughuli pia katika Uganda, Rwanda na Kenya[124]. Eneo lililo chini ya udhibiti wa kampuni hiyo katika Tanzania ni hekta 14,000 lakini wana lengo la kuwa na karibu hekta 24,000. Wanapanda miti kwa ajili ya kuhifadhi hewa ukaa kwa muda.
SFI Tanzania ni kampuni ya mashamba makubwa ya mkonge na miti, inayomilikiwa na kampuni ya Uholanzi ya the Dutch Form International, ambayo inaungwa mkono na serikali ya Uholanzi[125]. Mashamba makubwa ya mkonge na miti yanafunika eneo la zaidi ya hekta 3,000, kati ya hekta 6000 inazozidhibiti.

Kusoma zaidi
- Mashamba ya hewa ukaa ya Green Resources nchini Tanzania. Laana au tiba?
http://www.redd-monitor.org/2012/05/02/green-resources-carbon-plantations-in-tanzania-curse-or-cure

Mashamba makubwa ya mti ya CDM ya kuhifadhi hewa ukaa katika Afrika: Uchunguzi kifani katika Tanzania
http://wrm.org.uy/other-relevant-information/cdm-carbon-sink-tree-plantations-in-africa-a-case-study-in-tanzania

121 www.sifi.se/wp-content/uploads/2012/02/Forest-plantations-and-woodlots-in-Tanzania.pdf
122 www.redd-monitor.org/2012/05/02/green-resources-carbon-plantations-in-tanzania-curse-or-cure
123 http://kvtc-tz.com
124 www.unepfi.org/fileadmin/events/oversize/2010Joburg_Sullivan.pdf
125 www.forminternational.nl/form-ghana/#sthash.U8LHAZGs.dpuf

10) Uganda

Kama ilivyo katika Tanzania na Kenya, sera za serikali katika Uganda zilibadilika ili kukuza ushiriki wa biashara binafsi katika mashamba makubwa ya miti. Mkakati wa Mashamba Makubwa wa Mamlaka ya Taifa ya Misitu (NFA) ulipitishwa mwaka 2005, ukiweka akiba ya hekta 200,000 za Hifadhi Kuu ya Misitu (CFRs) kwa ajili ya mashamba ya miti. Hekta 50,000 lazima zipandwe na NFA na hekta 150,000 na wakulima binafsi.

Mpango wa kusaidia uzalishaji wa magogo ya kuchana mbao (SPGS) ulianza kama mpango wa pamoja kati ya Serikali ya Uganda na Umoja wa Ulaya (EU), na baadaye uliungwa mkono na Serikali ya Norway. Ulikuwa na nia ya kusaidia wakulima binafsi wa miti. Katika awamu ya kwanza ya mradi kulikuwa na ongezeko la shauku la mashamba makubwa ya miti katika Uganda[126]. Kupitia SPGS, NFA na sekta binafsi wamekuwa ndiyo wapandaji wakuu wa miti katika kipindi cha mwaka 2005-2010. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2010, nchi ilikuwa na jumla ya hekta 62,230 mashamba makubwa ya misitu. NFA ilikuwa na jumla ya hekta 14,140 sawa na (23%) wakati sekta binafsi ilimiliki hekta 48090 sawa na (77%). Hata hivyo, ripoti za hivi karibuni za FAO zinatoa takwimu za hekta 60,000 kwa mwaka 2015. Miti mikuu iliyopandwa ni misindano (*Pinus caribaea)* (kwa kwa ajili ya kuchana magogo ya mbao) na mikaratusi (*Eucalyptus grandis)* kwa ajili ya fito.

Nani ambaye anakuza mashamba makubwa ya miti nchini Uganda?

New Forest Company: Ina karibu hekta 21,500 za mashamba makubwa ya fidia/kusawazisha hewa ukaa katika maeneo matatu (mawili katika maeneo ya Hifadhi Kuu ya Taifa ya Misitu - na moja eneo binafsi) katika Wilaya za Mubende, Kiboga, Kyankwanzi na Bugiri. Kampuni imesababisha migogoro na wanajamii. Mara tu baada ya kampuni kuthibitishwa na FSC, zaidi ya watu 22,000 walifukuzwa kutoka ardhi zao na New Forest Company.

Green Resources Ltd: Wao wanapanda katika maeneo mawili ya Hifadhi Kuu ya Taifa - Bukaleba na Kachung - na wao wana karibu ya hekta 10,000 za mashamba makubwa ya miti vamizi hasa mikaratusi ambayo yamethibitishwa kama "misitu iliyosimamiwa kwa kuwajibika" na FSC. Kuna kashfa inayojikusanya juu ya uuzaji wa ongezeko la hewa ukaa za mpango Safi wa Maendeleo (CDM) ambazo 'hazipo' ambazo zilikuwa zipatikane kwa Green Rasilimali kutokana na mradi wake wa Kachung, kwenda kwa Wakala wa Nishati wa Sweden (SEA). [127]

Global Woods: ilianzishwa na mfuko wa Ujerumani, lakini sasa inamilikiwa na GEF yenye makao yake Marekani. Kati ya hekta zao 12,182 katika Kikonda CFR, hekta 8000 zimepandwa misindano na mikaratusi.[128]

Nile Plywood Ltd katika Kusini mwa Busoga imepanda hekta 1,500 ha za mashamba ya misindano

Kusoma zaidi

- Mashamba makubwa ya kimataifa ya timbao katika Uganda: Miti dhidi ya chakula www.redd-monitor.org/2016/01/08/global-woods-plantations-in-uganda-trees-versus-food
- Kampuni Mpya ya Misitu na mashamba yake makubwa katika uganda – Utafiti kifani wa Oxfam. www.oxfam.org/sites/www.oxfam.org/files/cs-new-forest-company-uganda-plantations- 220911-en.pdf
- Upande wenye giza zaidi wa kijani – Mashamba makubwa ya misitu na fujo za hewa ukaa nchini Uganda. www.oaklandinstitute.org/sites/oaklandinstitute.org/files/Report_DarkerSideofGreen_hirez.pdf
- Wakulima wa Uganda wafukuzwa katika ardhi yao ili kupisha mradi wa hewa ukaa wa Kampuni mpya ya Misitu http://www.redd-monitor.org/2011/09/23/ugandan-farmers-kicked-off-their-land-for-new-forests-companys-carbon-project

126 www.sifi.se/wp-content/uploads/2012/02/Forest-plantations-and-woodlots-in-Uganda.pdf

127 www.redd-monitor.org/2016/03/11/ngos-call-for-the-swedish-energy-agency-to-cancel-carbon-credit-purchase-from-green-resources-monoculture-plantations-in-uganda

128 www.globalenvironmentfund.com/global-woods

d. 11) Madagascar (Mashariki)

Takwimu za karibuni za FAO (FRA2015) zinaonyesha kwamba eneo la mashamba makubwa ya miti katika Madagascar ni karibia hekta 312,000. Hata hivyo, eneo lililokadiriwa katika mwaka 2000 lilikuwa juu zaidi karibia hekta 350,000, ambazo hekta 150,000 zilikuwa za mashamba makubwa ya mikaratusi yaliyoanzishwa mwanzoni mwa karne ya 20[129]. Miti iliyopandwa ni pamoja na mikaratusi, migunga (acacia), mvinje, misindano na aina nyingine za miti yenye majani mapana [130].

Mwaka 2005, FAO[131] iliripoti eneo la mashamba makubwa ya miti kuwa ni hekta 140,980, mashamba makubwa ya mikaratusi hekta 150,397, na "vichaka" hekta 1756,919, labda ikiwa ni pamoja na baadhi ya maeneo ya miti mgeni vamizi ambayo ilikuwa imeenea kutoka kwenye mashamba yaliyotelekezwa au kusimamiwa vibaya.

Madagascar ina historia ya utata juu ya upandaji wa mikaratusi[132], ambayo ilikuwa ya kwanza kupandwa na walowezi wa Kifaransa katika karne ya 19. "Mingi ya msitu ya awali ya asili ya Madagascar imebadilishwa na Mikaratusi, na kutishia bioanuai kwa kuyatenga maeneo ya asili yaliyobaki kama vile Andasibe-Mantadia National Park".[133]

Nani anayekuza mashamba makubwa ya miti mpya?

Mada Woodlands: Ni kampuni ya Norway yenye uzoefu wa usimamizi wa mashamba makubwa katika nchi za Nordic. Ina mipango ya kuanzisha hekta 50,000 za mashamba makubwa ya mikaratusi na migunga (acacia) mkoani Sofia, kwa uzalishaji wa mbao na hewa ukaa inayoongezeka[134].

WWF Madagascar: Hii NGO ya kimataifa inayounga mkono kwa dhati upandaji wa miti ya kigeni katika mashamba makubwa[135] kama njia ya kuondoa shinikizo la misitu ambayo inamalizika kwasababu ya mbao zinazotumiwa na watu wa ndani kwa ajili ya uzalishaji wa mkaa, na kusafishwa kwa ajili ya kupanda mazao. Tovuti yao inasema kwamba miti 800,000 ya migunga (acacia) na mikaratusi imepandwa. Ingawa hii inawakilisha eneo la takriban hekta 1,000 tu kwa jumla, ambazo pengine zingelikuwa zimetengenezwa na mamia ya vitalu vidogodogo vya miti, vilivyopandwa katika eneo kubwa, ambavyo vinaweza pia kusababisha matatizo ya mazingira katika siku zijazo, vinavyozidi kuenea.

Kusoma zaidi

- **Uporaji wa ardhi katika Madagascar: miangwi na shuhuda kutoka kondeni - 2013**
  www.recommon.org/eng/land-grabs-madagascar-voices-ground-2013-report-launch

- **Changamoto za utawala wa misitu katika Madagascar**
  https://www.umich.edu/~ifri/Publications/R051-31.pdf

- **Andrew Lees – Miaka 20 baada ya ujumbe wake nchini Madagascar**
- http://www.theecologist.org/campaigning/2625160/andrew_lees_20_years_after_his_last_mission_to_madagascar.html

129 http://www.wildmadagascar.org/overview/plantations.html
130 http://www.wildmadagascar.org/overview/plantations.html
131 http://www.fao.org/docrep/013/al556F/al556F.pdf
13 http://ur-forets-societes.cirad.fr/content/download/4468/35947/version/1/file/BFT323-No+to+the+Eucalyptus+war+in+Madagascar.pdf
133 http://eol.org/pages/29916/overview
134 http://www.recommon.org/eng/land-grabs-madagascar-voices-ground-2013-report-launch
135 http://www.wwf.mg/?202480/900000-trees

Shirika la Vuguvugu la Misitu ya Mvua Duniani yaani The World Rainforest Movement (WRM) inawezesha, inasaidia na kutia nguvu za harakati dhidi ya ukataji miti ovyo na kupora ardhi katika nchi zenye misitu na jamii zinazotegemea misitu. WRM pia huanika na kupinga mipango ya kimataifa na sera ambazo zinawasilishwa kama ufumbuzi wa kusimamisha au kubadili ukataji ovyo wa miti, lakini ambayo katika hali halisi hushindwa kuhifadhi misitu, na kupuuza madai na uchambuzi wa jamii zinazotegemea msitu kuhusu sababu za msingi za kupotea kwa msitu.

Kwa taarifa zaidi, tembelea www.wrm.org.uy

Shirika la Waangalizi wa Maswala ya Mbao yaani the Timberwatch Coalition (TW) ni umoja wa mashirika ya kiraia na watu binafsi ambao wanaguswa na madhara hasi ya kijamii na mazingira ya mashamba makubwa ya miti kwa ajili ya viwanda katika kusini mwa Afrika na kwingineko. Timberwatch inafanya kazi ya kuongeza uelewa wa athari hizi hatari, na inatia moyo jamii kupinga upanuzi wa mashamba makubwa katika kanda zao. TW pia inapinga ufumbuzi wa uongo kwa matatizo kama ya ukataji miti ovyo na mabadiliko ya tabianchi, kama vile fidia za kaboni, biashara ya utoaji wa hewa, nishati, na miradi ya uthibitishaji wa mashamba makubwa ya miti.

Kwa taarifa zaidi, tembelea www.timberwatch.org